Makala ya Mjadala wa Falsafa ya Kimapinduzi:

Demokrasi na Harakati za Kitabaka

na

Mwandawiro Mghanga

Bila nadharia ya kimapinduzi hapawezi kuwa na harakati za kimapinduzi – Karl Marx, Fredrick Engels na Vladmir Lenin

1. Utangulizi

Sema Usiogope Kusema Sema!

Ewe mwananchi mwenzangu
Ni nini kinakusumbua?
Lipi linakukera na kukukereketa mkereketo?
Yapi unayameza?
Sema
Wewe ni mwananchi
Una haki ya kusema sema
U raia wa Kenya kama wao
Tekeleza uhuru wako wa kutoa maoni sema
Simama wima na madhubuti
Usiyumbeyumbe kwa hofu usitetemeke
Sema tu bila woga
Wala usikubali utamaduni wa kimya na kutii kikondoo
Sema ukweli wako wote, wote kabisa
Mbona unawaruhusu wakufunge hata mdomo?
Kwa nini unawakubali wakukate ulimi wako?
Sema kile unachotaka kukisema
Kwa yule unaetaka kumsemea
Jinsi unavyotaka kukisema wewe
Na tena sema leo hii hii tu
Usingoje hadi kesho
Kwani watakuja kusema hukusema
Kataa sheria zao dhalimu za kukunyamazisha
Gomea kufugwa kama kondoo
Pambania haki yako ya kusema sasa
Potelea mbali kufa ni siku moja sema
Utawaogopa hadi lini?
Wao ni nani?
Sio watu kama wewe?
Mbona unachuja na kuchekecha maneno yako
Kwa ajili yao?
Usikubali ndugu usikubali

Mwananchi
Hata ikiwa huna inchi ya nchi yetu leo
Kataa katakata kataa kufanywa mtumwa
Usikubali wakuvue hata utu wako
Utawaabudu kama Mungu hadi siku gani?
Njoo haraka njoo mtu mwenzetu
Njoo tuungane tuseme kwa kauli moja:
Tutasema tutasema tumeamua tutasema
Tumegomea kunyamazishwa
Tumeasi utawala wa kiimla
Tumesema yametosha
Leo na sisi tutasema
Kwa vyovyote vile hatutakaa kimya
Kenya ni yetu sote
Sote ni wananchi
Sote ni raia hakika, sisi sote ni watu, binadamu
Kwa nini waseme wao kila siku
Na sisi tutii tu
Tutii tu siku zote tusiseme
Kama watumwa ama wanyama wa kufugwa?
Tutii tu siku zote tusiseme
La, hapana!
Potelea mbali!
Tutasema
Hata sisi lazima tuseme
Na wakitukataza
Haki yetu ya kusema
Tuseme
Tupambanie kusema

Mwandawiro Mghanga
Jela ya Kibos 24/9/1988

1.1. Wananchi wanadai demokrasi

Tumeamua kuanza majadiliano yetu kuhusu mapambano ya ukombozi wa kijamii na kitaifa nchini kwa kujaribu kuelewa na kufafanua maana ya demokrasi. Tumekata shauri kufanya hivyo tukizingatia kwamba hivi sasa harakati za kidemokrasi zinaendelea nchini Kenya na Afrika, ambalo hakika ni bara linalochemka kwa mapambano ya ukombozi kutoka kwa utawala wa kimla, ubeberu na unyanyasaji wa mtu kwa mtu.

Wananchi wengi wanadai mageuzi. Wamechoka na kuendelea kunyonywa, kutawalwa kwa mabavu, kuishi kwa hofu na wasiwasi katika nchi yao wenyewe. Wamechoka na maisha ya umaskini na ukosefu wa kila aina. Wemechoka na kugeuzwa watumwa au kufanywa wanyama wa kufugwa katika nchi zao wenyewe. Hawataki kuendelea kuwa chini ya uongozi wa mwenye nguvu mpishe mnyonge msonge. Wanataka mageuzi ya kuboresha hali ya wengi, mabadiliko ya kuleta mfumo wa kuhakikisha ukweli na haki, unaoheshimu utu wa kila mtu. Wanadai siasa mpya zitakazoweza kuwatanzua kutoka kwa silisili za ukoloni-mamboleo na kuwaelekeza mkondo wa kimaendeleo na maendeleo, barabara ya uhuru na kuboresha maisha.

Historia ya Kenya inaonyesha wazi kila siku ukweli huu. Wakenya wanadai demokrasi, wanaipigania usiku na mchana. Wananchi wengi wanaichukia serikali ya sasa kwa kuwa inapinga uhuru wao na wa taifa lao. Lakini vilevile inaonekana dhahiri shahiri kwamba kuna haja kubwa ya kujadiliana kuhusu maana ya demokrasi, hasa tukizingatia hali halisi katika nchi yetu na ulimwenguni leo uliyokumbwa na itikadi ya utandawazi wa kibeberu.

1.2. Umuhimu wa kufahamu maana ya demokrasi

Insha hii ni mchango wangu wa mjadala kuhusu swala nyeti la demokrasi. Katika insha yenyewe, ninakusudia kuchochea mjadala kuhusu demokrasi kuelekea kwa mkondo ufuatao:

Umuhimu wa kufahamu maana ya demokrasi: Usipofahamu maana ya kitu chochote kile, utakieleza kwa kutumia maana ya watu wengine ambayo huenda ikawa si ile unayoikusudia wewe mwenyewe na isitoshe iliyojawa na masilahi isiyo yako. Kwani kwa kila jambo, dhana au hali duniani, kuna mitazamo tofautitofauti na mingine inayokinzana. Vilevile kuna ukweli na uongo. Uongo unaweza kutokana na kutofahamu na aidha na makisudi ya kulinda masilahi fulani finyu, mara nyingi ya kitabaka.

Aidha, watu kutoka tabaka mbalimbali ama ambao wana mitazamo tofauti ya kitabaka, hufafanua dhana halisi kufungamana na mitazamo yao ya kitabaka ama imani ya kutetea ama kuwakilisha masilahi maalumu ya kibinafsi na ya kitabaka.

Kutokana na ukweli huu, tukiwa wananchi wazalendo, ambao tunapigania kujenga, kuikuza na kuiendeleza demokrasi, tutakosea tukikubali kufafanuliwa demokrasi, ama dhana yoyote ile na watu wengine, hata wawe wazuri na wenye nia bora kiasi gani. Kufahamu maana ya demokrasi ni hatua kubwa isiyoweza kuepukika ya kushiriki kikamilifu katika harakati za ukombozi wa kijamii na kitaifa. Chambilecho waanzilishi wa usoshalisti wa kisayansi, ”Pasina nadharia ya kimapinduzi hapawezi kuwepo na harakati za kimapinduzi”.

1.2.1. Hatari ya kufafanuliwa demokrasi na maadui

Hakika ni hatari kubwa mno kukubali kutegemea maana ya demokrasi ya watawala wa leo wa Kenya, watu kutoka tabaka la wenye mali, wasomi wenye mitazamo ya kibepari ama kisabili na hususani mabeberu. Lazima sisi wenyewe, wananchi binafsi, tukiwa kwa makundi ama kwa vyama, tujitahidi kutafiti na kutoka na maana yetu wenyewe kuhusu demokrasi: maana ya demokrasi itakayotusaidia kupigania na kujenga jamii ya kimaendeleo, inayohakikishia kila mwananchi haki ya kutekeleza haki zake kama mwananchi na kama binadamu. Na ili kufanya hivyo, lazima kila wakati tuchukue msimamo wa kitabaka. Tusipochukua msimamo wa kitabaka wa kutazama na kufahamu kila hali au dhana, basi tutadanganywa na kudanganyika, tutachanganyikiwa na kisha tutapotea njia ya ukombozi, tutatekwa nyara na kasumba ya maadui wetu. Tunaweza kujikuta katika hali ambapo tunadhani tunapambania demokrasi na haki za binadamu kumbe tunaupalilia na kuutilia mbolea mfumo wa ubepari na ukoloni-mamboleo.

1.2.2. Hatuwezi kuipigania demokrasi kikamilifu ikiwa hatuielewi

Jukumu muhimu la kila mzalendo na mwanamapinduzi ni kuipigania, kuilinda na kuiendeleza demokrasi katika jamii. Ila hatuwezi kuitetea ama kuipigania kikamilifu demokrasi ikiwa hatuielewi ipasavyo. Aidha, tusipoelewa kikamilifu kile tunachokipambania hatuwezi kukamilisha lengo la mapambano yetu kikamilifu. Tunaweza kujikuta, kwa mfano, tukipigania ubeberu na utawala wa wanyonyaji na madikteta wapya huku tukidhani tunapigania demokrasi katika nchi

yetu. Tunaweza kutumiwa kusaidia maadui wetu kukamata hatamu za serikali za kutunyonya na kutugandamiza na kutushindilia katika mashimo ya ubeberu wa kimataifa. Tunaweza kufanywa kupambana dhidi ya mawazo ya ukombozi wetu wenyewe kwa jina la demokrasi na haki za binadamu. Tunakariri, tunaweza kuingia katika mtego wa kuupalalia na kuutilia mbolea mfumo unaotunyonya na kutufukarisha huku tukifikiri tunapigania uhuru na haki za binadamu! Tutajaribu kuyafafanua haya yote kwa marefu na mapana katika insha hii na katika mazungumzo yenyewe.

1.3. Demokrasi ina historia

Bila kulewa tunatoka wapi hatuwezi kufahamu kikamilifu tuko wapi wala hatuwezi kubashiri ipasavyo tunakoenda. Kwa maneno mengine, ili kufahamu kikamilifu kitu chochote au dhana yoyote lazima tuelewe historia yake ya jana na leo. Tuelewe jinsi hali ilivyo kuwa hapo awali na ilikwendakwendaje hadi ikawa jinsi ilivyo leo. Tukiweza kufanya hivyo tutakuwa tayari kufanya mipango mizuri ya siku za usoni. Kwani jana, leo na kesho ni mambo ambayo yanahusiana katika hali ya mwendo wa wakati. Njia hii ya kuchambua matokeo katika jamii ndiyo inayojulikana kama uyakinifu wa kihistoria.

Basi katika insha hii, tukitumia njia ya uyakinifu wa kihistoria, tutajaribu kuelekeza mjadala huu kuona kuwa demokrasi ni dhana iliyo hai. Demokrasi si dhana iliyosimama, ni dhana inayotembea, inayokua na kubadilika. Demokrasi ni dhana yenye maisha ya jana na leo, yenye historia katika hali hasisi ya kijamii. Ni muhimu sana kuelewa jambo hili kwani wakati watu wa Kenya tukiwa katika harakati za kujenga mfumo wa kidemokrasi, tunakabiliwa na walimu wa demokrasi wanaojitahidi kutufundisha eti mifano ya kidemokrasi inapatikana tu katika nchi za kibepari na kibeberu, au zile zinazofuata mfumo wa ubepari.

Tunaambiwa ati tukitaka kujenga demokrasi Kenya, basi hatuna budi ila kufuata nyayo za serikali za nchi za Ulaya Magharibi ambazo ati ndizo serikali za kidemokrasi. Mawazo haya ya kibepari na kibeberu kuhusu demokrasi yanaenezwa na vyombo vya propaganda vya kibeberu nchini, balozi za nchi za kibepari, mabepari-uchwara wa kienyeji, na usomi na wasomi wa kisabili na mlengo wa kulia. Sababu ya nchi za kibeberu kutilia manani kudhamini Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (MYK) ni kujenga vyombo vya kutumika kueneza itikadi ya kibepari na kibeberu nchini, mkiwemo kuhusu demokrasi. Kwani mabeberu kila wakati wanaunda njama za kuteka nyara harakati za ukombozi zinazoendelea kote ulimwenguni. Nayo MYK yanayotegemea fedha za mabeberu yanatumiwa kuuimarisha ubepari na ubeberu nchini na ulimwenguni kwa jina la demokrasi, haki za binadamu, usawa wa kijinsia, kuhifadhi mazingira, masilahi ya vijana, n.k. Almradi ubeberu unatumia mbinu za kugawanya wanaonyonywa na kunyanyaswa katika jamii kimakundimakundi ili kuvunja umoja wao wa kupigania ukombozi wao.

1.4. Mawazo ya kibepari kuhusu demokrasi

Nadharia ya kidemokrasi ya kibepari ndiyo inayoshikiliwa na vyama vya upinzani vya Kenya ambavyo vimesajiliwa na serikali Moi-Kanu hadi wa sasa. Idadi kubwa ya mawakili wanaosema wanapigania demokrasi na haki za binadamu, wasomi wa mtazamo wa kibepari, mabepari wa kienyeji, viongozi wa dini, n.k., wote wanaongozwa na nadharia ya demokrasi ya kibepari katika harakati wanazoshiriki sasa.

Nadharia ya kidemokrasi ya kibepari ndiyo inayojulikana zaidi na wananchi wa Kenya kwani hawajapewa nafasi ya kujua ukweli hasa kuhusu demokrasi, tangu enzi za ukoloni wa Wingereza nchini, awamu ya Kenyatta na hii ya Moi. Wananchi wa Kenya tunafundishwa

kukubali uongo kuwa demokrasi inapatikana tu katika ubepari na kwamba demokrasi haiwezi kupatikana katika usoshalisti. Hata mataifa ya kibepari hujiita eti mataifa ya kidemokrasi na mataifa ya kisoshalisti huitwa eti mataifa ya kiimla. Vyombo vya habari nchini vinaeneza uongo huu usiku na mchana. Vinafanya hivyo kwa maksudi kwani vyenyewe vinamilikiwa na mabepari wa nchini na wa kutoka nje. Sera zao ni kulinda mfumo wa unyonyaji wa mtu kwa mtu huku zikijifanya kupasha habari, kufundisha na kutumbuiza. Na kila mara mabepari hutumia kila njia, mkiwemo redio, televisheni, magazeti, dini, n.k., 'kufundisha' umma ati hakuna mfumo wowote bora duniani kuliko wa ubepari. Na katika kufanya hivyo lazima wazue uongo wa kuupaka matope mfumo unaopinga ule wa ubepari, usoshalisti. Hii si ajabu kwani ni kanuni ya ubepari tangu kale na zamani.

Kwa maneno mengine, wananchi wengi wa Kenya tunaonyonywa na kugandamizwa, na ambao tunalilia na kupigania uhuru wetu, tunaelekezwa kufikiri kuwa tunaweza kuwa na demokrasi chini ya mfumo wa ubepari na ukoloni-mamboleo. Mawazo ya kibepari kuhusu demokrasi ndiyo yanayotawala ulimwenguni hivi leo chini ya utandawazi wa ubepari. Wakomunisti na wapenda maendeleo kote ulimwenguni wanashiriki katika harakati za kupambana dhidi ya utandawazi wa kibepari ambao pia unahimiliwa na demokrasi ya kibepari. Mawazo ya kibepari kuhusu demokrasi yanakusudiwa kudanganya wananchi wengi kuwa kile kinachopinga uhuru na demokrasi Kenya ni udikteta wa Moi na Kanu peke yake, wala siyo mfumo wote wa kijamii-kiuchumi wa ubepari wa kikolonimamboleo. Kwa mfano, mengi ya MYK nchini yanaongozwa na mawazo yanayoshikilia ati ubeberu ni rafiki wa harakati za ukombozi wa kijamii na kitaifa, ati dola za kibepari na kibeberu zinaweza kusaidia umma unaonyonywa na kugandamizwa kujikomboa. Katika insha hii tutashiriki katika mapambano dhidi nadharia ya kibepari kuhusu demokrasi inayotumiwa kurubuni wengi wanaonyonywa na kugandamizwa.

1.5. Demokrasi ni sehemu ya harakati za kitabaka

Aidha, tutajaribu kuthibitisha kwa mifano halisi katika nchi yetu kuwa siyo tu kwamba demokrasi ni dhana yenye historia katika jamii halisi, bali pia kila penye mfumo wa kitabaka demokrasi vilevile hudhihirisha makinzano ya kitabaka. Matabaka mawili tofauti hayawezi kuwa na haki sawa wakati mmoja.

Madai ya mawazo ya kibepari kuhusu demokrasi kuwa waajiri na waajiriwa wanaweza kuwa na haki sawa za kidemokrasi wakati mmoja, ati maskini na matajiri wanatekeleza haki za kidemokrasi sawasawa katika nchi za kibepari ni uongo unaoonekana wazi katika hali halisi ya maisha ya kila siku.

Nchini Kenya, kwa mfano, demokrasi inayopiganiwa na matajiri si sawa na ile inayopiganiwa na maskini. Matarajio ya wafanyikazi kuhusu demokrasi si sawa na yale ya waajiri. Wakati maskwata na wakulima makabwela wanadai demokrasi itakayowapa haki ya kuwa na ardhi, wenye ukiritimba wa maelfu ya maeka ya ardhi wananataka demokrasi itakayolinda ukiritimba wao juu ya ardhi. Mwenye mali na asie na mali hawawezi kuwa na haki sawa za kidemokrasi. Huu ni ukweli wa historia ya leo, ya zamani na ya siku za usoni.

1.6. Mbinu za kupambana dhidi ya udikteta

Ni kweli kabisa kwamba hivi sasa katika nchi yetu udikteta wa Moi-Kanu, ni udikteta wa watu wachache kabisa ambao unawanyanyasa hata watu wa tabaka lake, tabaka la matajiri na mabepari wa kienyeji.

Hii ndiyo sababu karibu ya vyama vyote vya upinzani vilivyosajiliwa vinaongozwa na watu wanaotoka kwa tabaka linalotawala (ambalo pia ni tabaka la kina Moi na waitifaki wake), mamilionea wa kienyeji, wafanyibiashara, wabakuzi wa mashamba na maploti mijini, mawakili wa siasa za mlengo wa kulia, wasabili wa kila aina na wale wote wanaokusudia kuuondoa utawala wa Moi-Kanu na kuubakisha mfumo wenye msingi wa udikteta na unyonyaji, ubepari wa ukolonimamboleo.

Bali hii si kusema kwamba hivi sasa sisi watu wa tabaka la wengi wasiyo na mali hatuwezi kushirikiana na wale wa tabaka la wachache wenye mali (wanyonyaji) kupambana dhidi ya udikteta wa Moi-Kanu ambao sasa u kikwazo kikubwa zaidi kwa hatua yoyote mbele ya kidemokrasi. Kinyume chake, tunatoa mwito kwa vyama vyote vya upinzani vifanye mshikamano dhidi ya imla ya Moi-Kanu.

Meli ya kuung'oa utawala wa imla ina nafasi kwa watu tabaka zote nchini. Wala haibagui abiria yoyote anaetaka kusafiri kwa meli hii. Kile tunachokifahamu ni kwamba ingawa safari yetu ya demokrasi imetukutanisha kwa meli moja abiria kutoka kwa matabaka mbalimbali, ukweli ni kwamba mwanzo na mwisho wa safari yetu haufanani.

Safari ya abiria wachache, wa kutoka kwa tabaka la matajiri, ni fupi sana. Ikienda mbali zaidi itaishia kwa kuangushwa kwa udikteta wa Moi-Kanu ambao kamwe hauwezi kuepukika hivi punde tu. Bali safari ya sisi abiria tuliyo wengi, sisi wa tabaka lisilo na mali, tunaotoka kwa walalahoi, ni ya mbali sana na tena ni ngumu mno. Kwani tunaona udikteta wa Moi-Kanu kuwa kikwazo tu cha kuelekea kwa kazi ngumu zaidi ya kujenga demokrasi ya umma. Na kujenga demokrasi ya umma ni kupambana dhidi ya ubepari na ubeberu.

Lengo letu la hatimaye la demokrasi ya umma ni kuung'oa kabisa mfumo wa unyonyaji wa mtu kwa mtu, ambao ndiyo msingi hasa wa udikteta wa watu wachache dhidi ya watu wengi. Kwa hivyo, tukiwa kwa meli hii ya kuelekea kwa demokrasi, tujitahadhari sana tusije tukashuka bandari moja na maadui wetu wa kitabaka. Tena tusiwaamini hata kidogo wa kutoka kwa tabaka la wanyonyaji ati kwa kuwa hivi sasa sote tunapambana dhidi ya udikteta wa Moi-Kanu. Wanaweza kutupoteza njia ama kututupa baharini tukaliwa na papa wa ubepari na ubeberu.

Isitoshe, hata uchungu wa kuumizwa na udikteta si sawa. Uchungu wetu sisi wa tabaka la maskini ni mkubwa zaidi, tunanyanyaswa mara nyingi zaidi kuwaliko matajiri, madugu wa kitabaka wa wenye kudhibiti vyombo vya dola. Kwa sababu hii, tuna haraka zaidi ya kufika mwisho wa safari ya mapambano ya kidemokrasi kuwaliko mabepari ama mabepari-uchwara.

1.7. Demokrasi haianguki kutoka mbinguni!

Katika insha hii vilevile, ninakusudia kufafanua ukweli kwamba kila hatua inayopigwa mbele kuelekea kwa demokrasi, imetokana na mapambano makali ya wanaonyanyaswa.

Katika historia, demokrasi haijawahi kuanguka kutoka mbinguni wala kupewa kama zawadi kwa wanaonyanyaswa. Demokrasi hutafutwa, hushughulikiwa, hupambaniwa, hupiganiwa, hunyakuliwa, hujengwa na juhudi za kizalendo na kimapinduzi. Hili ni rahisi sana kueleweka kwa Wakenya kwani historia yetu yenyewe inafafanua ukweli huu wazi na bayana.

Mapambano dhidi ya ukoloni-mkongwe, wa Wingereza, vilevile yalikuwa mapambano ya kidemokrasi nayo yalidai juhudi kali za kujitoa mhanga kutoka kwa wazalendo. Maelfu kwa maelfu ya mashujaa wa uhuru wa nchi yetu walikamatwa, waliteswa, walifungwa kizuizini,

walihamishwa, waliuawa wakipigania haki ya wananchi wa Kenya ya kujitawala na kujiamulia sudi yao wenyewe.

Kilele cha harakati za ukombozi wa nchi yetu kutoka kwa ukoloni-mkongwe kilikuwa vita vya kigorila vya Mau Mau. Kwa kujiita Jeshi la Uhuru na Mashamba, Mau Mau wanabainisha wazi kuwa walitambua kuwa jukumu lao kama wazalendo la kuwa katika msitari wa mbele wa vita vya kuhakikisha wananchi wa Kenya tutapiga hatua mbele ya kujitawala na kujiamulia maisha na mambo yetu kama taifa huku tukizingatia uchumi wa haki na maendeleo kwa wananchi wote. Na bila ardhi hapawezi kuwa na taifa.

Mnamo mwaka wa 1992, utawala wa Moi-Kanu ulilazimishwa na harakati za Wakenya kuondoa kifungo kilichokuwa kwa katiba ya kitaifa ya Kenya ambacho kiliingizwa kiharamu mnamo mwaka wa 1982 ili kuifanya Kenya kuwa chini ya imla ya chama kimoja, chama cha Kanu. Wakenya wengi walifungwa, waliteswa, walipoteza kazi zao na mali zao, walilazimika kutoroka nchi yao na kuishi uhamishoni, waliwekwa vizuizini, waliuawa, katika mapambano ya kuupinga mfumo wa chama kimoja.

Hatua ya kidemokrasi tuliyoipiga hadi sasa, ya kunyakua mfumo wa vyama vingi kikatiba, hata ingawa ni hatua ndogo sana na haijauondoa mfumo wa kiimla, ni hatua muhimu, ni hatua mbele. Nayo imetokana na mapambano makali ya wananchi ambayo bado yanaendelea. Mfumo wa vyama vingi haukuletwa na shinikizo za nchi za kigeni kama watu wengine wanavyodai, wala hatukupewa na dikteta Moi na genge lake. Mfumo wa vyama vingi ambao Wakenya wanaendelea kupambana kuuhami na kuuhifadhi umetokana na mapambano halisi ya wazalendo wa nchi yetu.

Kwa mantiki hii, tunaweza kusema pia utawala wa kishenzi na kinyama wa Moi-Kanu unaotupinga kusonga mbele kuelekea kwa uhuru na demokrasi utaangushwa na juhudi za mapambano ya wananchi wa Kenya wenyewe wala siyo na mabeberu ambao usiku na mchana wanajitahidi kuwadanganya watu wa Kenya kuwa wanataka kuona demokrasi katika nchi yetu, na wakati huo huo wanashirikiana na utawala wa Moi-Kanu kutunyonya na kutufukarisha kwa kila hali kama taifa. Chambilicho kiongozi wa mapinduzi ya Uchina, Komredi Mao Tse Tung, *mabeberu ni marafiki wanaokuja na asali mdomoni na mkuki mkononi*.

2. Ufafanuzi wa demokrasi

Baada ya kusema haya yote, hebu turudi kwa swali letu: demokrasi ni nini? Tukikumbuka haya niliyoyasema hapa juu, tutaelewa kuwa demokrasi kwa wale wenye kuwakilisha itikadi ya kibepari - itikadi ya tabaka la wenye mali, itikadi ya kibeberu - ni tofauti na demokrasi ya kutoka kwa wale wa itikadi ya kisoshalisti, ambayo ni itikadi ya tabaka la wengi wanaofanya kazi, wanaonyonywa, wanaopigania mageuzi ya kimsingi.

Demokrasi imewahi kufafanuliwa kama *serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa ajili ya watu*. Ufafanuzi huu ukitazamwa kijuujuu unaonekana unafaa sana. Lakini ukitazamwa kwa undani, ukihakikiwa na ukichambuliwa, jinsi tutakavyojaribu kufanya hivi sasa, itagunduliwa kwamba unaficha mengi, u pazia ya kuzuia kuonekana kwa harakati za kitabaka ambazo daima ni sehemu ya demokrasi.

Tunapoambiwa kuwa demokrasi ni serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa ajili ya watu, je, *ni nini maana ya watu katika ufafanuzi huu*? Kwani wakati Wayunani walipokuwa wakitumia neno demokrasi kwa mara ya kwanza hawakuwa na shaka yoyote kuwa watu walikuwa wale waliyokuwa wakitawala Uyunani wakati huo. Nao walikuwa ni tabaka la mabwana waliyokuwa

wakidhibiti njia kuu za uzalishaji, raia waliyokuwa huru na waliyokuwa wakimiliki watumwa. Kwa Wayunani enzi hizo, wale watu waliyotoka kwa tabaka la watumwa hawakuhesabiwa kuwa watu.

Je, *ni nini maana ya serika!i katika ufafanuzi huu wa demokrasi*? Kuna maana kuwa serikali i juu ya watu na kwamba ni ya watu wote katika jamii? Ni nini maana ya serikali?

3. Jamii ya mfumo wa umajumui

Sasa jamii peke yake katika historia ya binadamu ambapo mtu angeliweza kuzungumzia kuhusu watu kwa ujumla bila hofu yoyote ile ya kuonekana unaficha mambo fulani, ni jamii ya mfumo wa umajumui.

Kwani *katika mfumo wa umajumui jamii haikuwa imegawanyika kitabaka***.** Hapakuwa na tabaka la watawala na watawaliwa, wenye kumiliki njia kuu za uzalishaji mali na wale ambao hawakuwa na njia za uzalishaji, matajiri na maskini. Haya maovu yote hayakuwako. Mfumo wa umajumui ulikuwa mfumo wa usawa.

Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa katika mfumo wa umajumui, watu walikuwa nyuma sana kimaendeleo. Walikuwa katika ushenzi mkubwa mno. Kulingana na binadamu wa leo, pengo kati ya binadamu wa umajumui na wanyama lilikuwa kidogo mno.

Kwani binadamu wa umajumui walikuwa wanaishi katika maskani ya kishenzi kama juu ya miti ama kwa mapango. Walipata chakula kutokana na usasi wa kishenzi na kutokana na kuchuma matunda ya misituni na mizizi ya porini. Hawakuwa wameanza kutumia vifaa vyovyote vya maana wala hawakuwa wanafuga mimea na wanyama.

Kwa muhutasari, katika mfumo wa umajumui, binadamu alikuwa akitawalwa na maumbile, akiishi kwa huruma za maumbile kwani hakuwa anazifahamu na kuzidhibiti sheria zinazotawala maumbile. Katika hali hii kila mtu alihitajika katika jamii kwa ajili ya kazi ya kutafuta chakula na kujihami kutoka kwa maumbile. Wanawake na wanaume, na watoto pia, wote walishiriki katika kazi ya uwindaji na utafutaji matunda na mizizi ya porini kwa ajili ya chakula. Chochote kilichopatikana kiligawanywa kwa usawa kufungamana na wingi au uchache wa chakula chenyewe na mahitaji ya kila mtu.

Basi kutokana na uzalishaji na umilikaji wa pamoja wa kile kilichozalishwa, jamii ya mfumo wa umajumui ilikuwa ya usawa na wala haikuwa na matabaka. Na kwa sababu hapakuwa na mataba vilevile hapakuwako na harakati za kitabaka. Na kutokuwa na harakati kitabaka kuna maana kuwa katika mfumo wa umajumui hapakuwa na dola kwa kuwa halikuhitajika.

Tukifuata mantiki hiyo hiyo, ikiwa demokrasi ni serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa ajili ya watu, basi tunaweza kudai kuwa hapakuwa na demokrasi katika mfumo wa umajumui, kwani, ijapokuwa kulikuwa na watu katika mfumo wa umajumui, hapakuwepo na dola ama serikali wakati huo huo. Na *kamwe haiwezekani kutenganisha demokrasi na dola.*

Ukweli huu, kwamba hapakuwepo na demokrasi katika mfumo wa mwanzo wa jamii ya binadamu, umajumui, utatusaidia kufahamu zaidi kuwa *demokrasi ina historia yake, kwamba demokrasi ni zao la mahusiano maalumu ya binadamu, inatekeleza shabaha maalumu na ilianza wakati ilihitajika katika jamii na wala hatuwezi kuitenganisha na dola wala harakati za kitabaka.*

4. Maana ya dola

Kufikia hapa ni muhimu tutulie kidogo ili tufafanue maana ya dola. Maana hakuna swala lililovurugwa kimaksudi na mabwanyenye na usomi wa kibwanyenye kama swala la dola. Njama za kuficha ukweli kuhusu dola zimekuwako tangu mwanzo wa dola. Zimekuwako nyakati za mfumo wa utumwa, ukabaila na ubepari. Katika enzi hizi za utandawazi wa ubeberu, ukweli kuhusu maana ya dola umefichwa hata zaidi. Kwa mfano, watu wengi wanafikiri ati dola ni sawa na serikali na wakati huohuo wanaamini ati ”serikali ni mimi na wewe”, ati serikali ni ya watu wote. Kuna dhana ati dola ni kama Mungu na iko kwa ajili ya kila mtu. Ati dola haipendelei tabaka lolote, kazi yake ni kuhakikisha amani, usalama, haki, utangamano na mema kwa kila mtu katika jamii pasina kujali tabaka, kabila, jinsia, au hali yoyote baina ya binadamu. Kuhusu chanzo cha dola inasemekana ati kulikuwako wakati ambapo binadamu hawakuwa na dola. Basi kukawa kuna vita, dhuluma, maovu na vinyang’anyiro vya kila aina. Wakati huo ati ”maisha yalikuwa magumu, ya kishenzi, hatari na mafupi”. Ili kusuluhisha jambo hili, ati binadamu walikutana na kufanya mkataba uliounda dola lenye jukumu la kuhakikisha usalama na amani ya watu na mali zao katika jamii. Mawazo kama haya bado yanaenezwa nchini na ulimwenguni.

Lakini je, ni nini ukweli kuhusu maana ya dola. Wakomunisti ndiyo wanaoeleza ukweli halisi kuhusu dola. Maana wakati ambapo ubepari unatumia uongo kama njia ya kujiendeleza, ukomunisti hauwezi kuendelea bila ukweli. Ndiyo kwa sababu ufafanuzi wa dola wa kikomunisti unaambatana na ukweli halisi katika maisha ya kila siku katika nchi yoyote ile. Tena bila kujua ukweli kuhusu dola hatuwezi kujua maana ya demokrasi na mapinduzi, hasa mapinduzi ya kishoshalisti.

Dola ni mashini ya tabaka moja ya kugandamiza tabaka lingine. Katika kutekeleza kazi yake ya ugandamizaji, mashini hii inayoitwa dola, hutumia vyombo vyake vya kuhofisha, kushawishi, kushurutisha na kunyanyasa. Vyombo hivi ni pamoja na sheria, polisi, magereza, majeshi, mahakama, serikali, n.k.

Katika mfumo wa umajumui, jamii haikuwa na tabaka lililokuwa likitawala, kunyonya na kunyanyasa tabaka lingine. Kwa sababu hii hapakuwa na haja ya vyombo vya dola vya kulazimisha tabaka moja kukubali utawala wa tabaka lingine.

Kwa mfano, kwa kuwa jamii ya umajumui, iliishi kwa usawa ambao ulilindwa na adili, miko na mila ambazo zilikubaliwa na kila mtu katika jamii hiyo, basi hapakuwa na haja ya sheria wala mahakama ya kuhukumu wale ambao walikataa kufuata sheria. Wala hapakuwa na polisi ama magereza ama majeshi ya kutekeleza sheria na hukumu za mahakimu. Hapakuwa na haja ya ma-PC, ma-DC, ma-DO, machifu na masabuchifu wa kutawala watu wengine na kuwashurutisha kufanya mambo fulani.

Haya yote yalianza kuonekana wakati jamii ilipokua na kuanza kugawanyika katika matabaka mbalimbali. *Dola na demokrasi ni zao la mfumo wa kwanza wa kitabaka.* Aidha demokrasi, kama dola vilevile, imekuwa ikikua kwa wingi na ubora jinsi jamii nayo imekuwa ikikua na kuendelea mbele kila wakati, ijapokuwa kwa mwendo upogoupogo.

5.1. Mfumo wa utumwa

Mfumo wa utumwa, ndiyo mfumo wa kwanza wa matabaka halisi ambao unajulikana katika historia. Katika mfumo huu, kulikuwa na tabaka la mabwana kwa upande mmoja na la watumwa kwa upande mwingine.

Njia kuu ya uzalishaji mali ilikuwa ardhi nayo ilikuwa imemilikiwa na tabaka la mabwana. Watumwa hawakuwa na umilikaji wa njia ya uzalishaji, kwani *watumwa wenyewe walikuwa mali ya tabaka la mabwana.*

Wakati wowote ule katika historia, katika mfumo wowote ule wa kitabaka, hali inakuwa kwamba tabaka moja linafurahia uhuru, demokrasi na haki za binadamu wakati ambapo tabaka lingine linaporwa uhuru, demokrasi na haki za binadamu.

Aidha, wakati wowote ule tabaka ambalo linadhibiti nguvu za dola na kumiliki njia kuu za uchumi, huwa ndilo tabaka linalotawala, huwa ndilo tabaka linalokula matunda ya uhuru na kufurahia haki za binadamu zaidi, huwa ndilo tabaka lenye kuhodhi utajiri na mali, huwa ndilo tabaka linalonufaika kutoka kwa maendeleo ya kitamaduni, ndilo tabaka linalonyonya na kudhulumu. Katika mfumo wa utumwa, tabaka hili lilikuwa la mabwana.

Tabaka la watumwa halikuwa huru, kwani watumwa walihesabiwa kuwa mifugo ya kutumiwa na mabwana zao. Haki za binadamu za watumwa hazikutambuliwa katika sheria ama mahakama ya jamii hii kwani hawakuhesabiwa kuwa binadamu. Watu huru, ama raia, kama walivyojulikana huko Uyunani, ndio waliokuwa na demokrasi. Watu kutoka kwa tabaka la mabwana, ndio waliokuwa huru kutoa maoni yao, kutembea na kukutana, kujitetea mahakamani, kukosoa serikali na jamii, kuchagua viongozi na kujadiliana kuhusu taratibu za utawala, falsafa, n.k.

Tabaka la mabwana huko Uyunani ndilo lililobuni neno demokrasi katika juhudi za kutafuta utaratibu bora wa utawala katika jamii yao. Na kwa mabwana utaratibu bora ulikuwa ni kulinda mfumo wa utumwa, wa unyanyasaji wa mtu kwa mtu. Kwa sababu hii, inaposemekana kuwa demokrasi ni serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa ajili ya watu, *Wayunani walikusudia kusema kwamba demokrasi ni serikali ya tabaka la mabwana inayoongozwa na watu kutoka tabaka la mabwana kwa ajili ya watu kutoka tabaka la mabwana.* Na kwa kuwa serikali katika mfumo wa utumwa ilikuwa ni chombo cha tabaka la mabwana cha kugandamiza tabaka la watumwa, basi demokrasi nayo ilikuwa inatekeleza kazi ya kuwanyonya na kuwanyanyasa watumwa.

Maamuzi yote yaliyofanywa kutokana na mijadala ya kidemokrasi katika mfumo wa utumwa yalikuwa kwa ajili ya watu kutoka tabaka la mbwana na wala siyo kwa ajili ya watu wote katika jamii, kwani tunakariri, *watumwa hawakuhesabiwa kuwa watu*. Demokrasi ilitekeleza kazi ya kuuimarisha mfumo wa utumwa. Nao mfumo wa utumwa ulikuwa ni wa kuwanyanyasa watumwa. Hivyo basi, katika mfumo wa utumwa, demokrasi ilitumiwa na tabaka la mabwana kudumisha mahusiano ya kuwanyanyasa watu kutoka tabaka la watumwa.

5.2. Harakati za kitabaka katika mfumo wa utumwa

Tumesema kuwa *kila kunapokuwapo na matabaka harakati za kitabaka nazo haziwezi kuepukika*. Katika mfumo wa utumwa, watumwa walikuwa wakipambana siku zote kwa njia mbalimbali dhidi ya nyanyaso za mabwana. Watumwa hawakukubali hali ya kunyonywa na kunyanyaswa. Kila mara walikuwa wakijitahidi kujikomboa kutoka kwa mfumo wa utumwa.

Tabaka la mabwana kwa upande wake lilitumia kila njia kuudumisha utawala wao wa kidhalimu na kinyonyaji dhidi ya tabaka la watumwa. *Dola la mfumo wa utumwa ambalo lilikuwa ni mashini ya tabaka la mabwana la kuwagandamiza tabaka la watumwa, lilikuwa na shabaha ya kuyahifadhi na kuyadumisha mahusiano ya kidhalimu ya utumwa.* Watumwa hawakuwa na demokrasi ya kuchagua ikiwa walitaka kuendelea kuwa watumwa au la. Hawakuwa na uhuru wa kusema, kusafiri, kujumuika au kupiga kura. Hawakutekeleza haki ya kuamua chochote kile maishani, hata kuhusu maisha yao yenyewe! Vyombo vya dola vilitumika kuwatawala na kuwalazimisha kuwa watumwa. Sheria, polisi, majeshi, magereza na serikali zilitumika kuvunja migomo yao ambayo ilikuwa ni sehemu ya maisha katika mfumo wa utumwa.

Makinzano kati ya kukua kwa nyenzo za uzalishaji na mahusiano ya kijamii ya kitumwa ambayo yalifikia hali ya kuwa kikwazo kwa kukua kwa nyenzo za uzalishaji, hatimaye yaliulazimisha mfumo wa utumwa kuupisha mfumo mpya, wa hali ya juu zaidi kwa kila hali kuliko ule wa utumwa. Mfumo huu unajulikana kama mfumo wa ukabaila[1].

6. Mfumo wa ukabaila

Katika mfumo wa ukabaila, kulikuwa na matabaka mawili makuu, tabaka la makabaila na lile la wajoli. Tabaka la makabaila ndilo lililokuwa tabaka tawala, ndilo lililomiliki njia kuu ya uzalishaji, ardhi; ndilo lililokuwa linahodhi utajiri wote katika jamii uwe wa mashamba, mifugo au uliyotokana na biashara; ndilo lililokuwa linadhibiti siasa, uchumi na nguvu za dola.

Tabaka la wajoli lilikuwa tabaka la kutawalwa, kunyonywa na kugandamizwa kwa kila hali. Wajoli walikuwa huru zaidi kulingana na watumwa. Kwani *wakati ambapo watumwa hawakuhesabiwa kuwa watu angalawa wajoli walikuwa wamenyakua haki ya kuhesabiwa kama watu.*

Hata hivyo, ingawa kulikuwa na tofauti sehemu mbalimbali ulimwenguni, kwa ujumla hali ya wajoli haikuwa tofauti sana na ya watumwa. Kwani wajoli hawakumiliki njia ya kujipatia riziki, ardhi. Kwa hivyo, iliwabidi waendelee kuishi kwa kunyonywa na kunyanyaswa na makabaila ambao ndio waliomiliki ardhi na rasilimali zote katika jamii. Wajoli walilazimika kuishi kama wafungwa katika mashamba ya makabaila, wakizalisha mazao ya kilimo ambayo yalinyakuliwa na makabaila huku wakiwachiwa kidogo tu kwa ajili ya kuwawezesha kuendelea kuwa hai ili waendelee kuwazalishia makabaila zaidi.

Dola lilidhibitiwa na tabaka la makabaila na lilikusudiwa kuyadumisha mahusiano ya kinyonyaji na kidhalimu ya mfumo wa ukabaila. Dola lilikuwa ni mashini ya tabaka la makabaila ya kugandamiza tabaka la wajoli. Serikali ilikuwa mikononi mwa wafalme au malkia. Taasisi ya ufalme au umalkia ilijengwa na kuimarishwa ili kuwakilisha na kulinda maslahi ya tabaka la makabaila na mfumo wa ukabaila.

Tunaweza kusema kwa muhtasari kwamba *katika ukabaila, demokrasi ilikuwa ni serikali ya makabaila iliyokuwa ikiongozwa na wafalme (au mamalkia) kwa ajili ya makabaila na wafalme (au mamalkia)*.

Demokrasi ilikuwa ikiwagandamiza wajoli. Vyombo vya dola, yaani ufalme, polisi, sheria, mahakama, magereza, majeshi, mamlaka mbalimbali ya serikali, vyote vilikuwa vinatekeleza kazi ya kuuimarisha utawala wa kifalme na kikabaila ili kupambana dhidi ya wajoli na wale wote waliokuwa wakidai mageuzi ya kuwakomboa kutoka kwa nyanyaso za mfumo wa ukabaila.

[1] Nimeyajadili na kuyafafanua haya kwa mapana na marefu katika insha *Uhuru na Haki za Binadamu*.

Kwani harakati za kitabaka zilikuwa sehemu ya historia ya ukabaila, kama ilivyo katika mfumo wowote ule wa kitabaka.

7. Jinsi mfumo wa ubepari ulivyozaliwa na mfumo wa ukabaila

Hata hivyo, msingi wa historia ya binadamu siyo harakati za kitabaka peke yake. *Kile kinachofanya historia, kinachosababisha maendeleo na mageuzi, msingi wake ni kukua kwa nyenzo za uzalishaji*[2]*. Harakati za kitabaka huchochea na kukamilisha mageuzi yanayoletwa na kukua kwa nyenzo za uzalishaji***.** Kwa maneno mengine, jinsi Fredrick Engels alivyoandika, *mapinduzi ni mkunga wa jamii kongwe ambayo ina mimba pevu ya jamii mpya*.

Katika karne ya kumi na tisa, huko Ulaya, ilikuwa wazi kwamba kilele cha makinzano kati ya nyenzo za uzalishaji na mahusiano ya uzalishaji ya kikabaila kilikuwa kimefika. *Maendeleo ya kiuchumi yalizaa tabaka lingine mpya, ambalo linaitwa tabaka la mabepari.*

Tabaka hili lilikuwa tabaka la wafanyibiashara, wenye viwanda na ambalo lilikuwa likipambana kujenga uchumi mpya wa biashara na viwanda, uchumi wa kibepari. Bali uchumi wa kibepari unahitaji wafanyikazi. Na tabaka peke yake ambalo lingetoa nguvukazi, ambalo lingewasilisha wafanyikazi waliokuwa wakihitajiwa na mabepari lilikuwa tabaka la wajoli.

Bali dola la ukabaila lilikuwa linazuia wajoli uhuru wa aina yoyote ile, hata wa kusafiri kwenda mijini ama kuchagua mabwana wa kuwafanyia kazi. Wajoli hawakuwa hata na haki ya kuchagua wataishi wapi au hata ni nani watamuuzia nguvukazi yao. Kwa sababu hii ukabaila ulikuwa ukipinga kuibuka kwa mfumo mpya wa kibepari ambao wakati wa kuibuka kwake ulikuwa umefika. Ukabaila ulikuwa unazuia ama kucheleweshe kukua kwa sayansi na tekinolojia ambayo ilikuwa inadai sehemu yake katika kujenga uchumi wa viwanda na biashara, wa kutumia maarifa yaliyozalishwa na wanasayansi na mafundi tilatila.

Tabaka la mabepari likawa linadai demokrasi na haki za binadamu. Harakati za kupigania uhuru, haki na usawa zikaenea. Mabepari na mkururo wa mabepari mchwara wakawa wanapambana dhidi ya ukabaila na ufalme, wakiwa na nia ya kuuangusha ukabaila na kujenga mfumo mpya wa hali ya juu zaidi badala yake, ubepari.

Ikawa basi tabaka la wajoli likashirikiana na tabaka la mabepari ambalo lilikuwa likichipuka, kupambana dhidi ya mfumo wa ukabaila. Mapambano ya wajoli na mabepari yaliuangusha mfumo wa ukabalila na kujenga mfumo wa ubepari. Mapinduzi ya kibepari yaliyotokea Ulaya mnamo karne ya kumi na tisa yakafanyika.

Mapinduzi ni mabadiliko kamili ambapo tabaka moja linanyakua nguvu za dola, kiuchumi na kisiasa kutoka kwa tabaka lingine. Ingawa mapinduzi ya kibepari yalisababishwa na mapambano ya wajoli wakishirikiana na mabepari, ni mapinduzi ya kibepari kwa sababu mabepari ndio walionyakua nguvu za dola, kisiasa na kiuchumi. Mabepari ndio waliofaidi zaidi kutokana na mapinduzi ya kibepari waliyoyafanya kwa kushirikiana na tabaka la wajoli. Jambo hili ni muhimu sana kukumbuka na kuzingatia. Kwani haitoshi kujitoa mhanga, hata mhanga hujitoa mhanga. Kila tunaposhiriki katika mapambano sharti tufahamu vizuri tunapambania nini, tunashirikiana na nani na hatima ya mapambano yenyewe ni nini. Ikiwa ni harakati za kidemokrasi tunazoshiriki, ni demokrasi gani, ya masilahi ya nini na nani? Na ili kufanya hivyo, sharti tuelewe historia ya nchi yetu na ulimwengu - tujue tutokako, tulipo na twendako - huku tukichukua msimamo wa kitabaka na kuongozwa na itikadi ya kimapinduzi, ukomunisti.

[2] Haya pia tunayafafanua katika *Uhuru na Haki za Binadamu.*

8. Demokrasi ya Kibepari

8.1. Maisha ya wafanyikazi baada ya mapinduzi ya kibepari

Baada ya mapinduzi ya kibepari, wajoli walijishindia uhuru zaidi, walijinyakulia haki nyingi zaidi kuliko hapo awali, wakati wa ukabaila. Lakini *mapinduzi ya kibepari hayakuwapatia wajoli haki ya umilikaji wa njia za uzalishaji mali*. *Isitoshe, vyombo vya dola vilikuwa vinadhibitiwa na mabepari* ambao vilevile ndiyo walikuwa watawala wapya wa siasa na uchumi.

Wajoli hawakumiliki ardhi, hawakumiliki viwanda wala biashara. Walipojikomboa kutoka kwa nyanyaso za ukabaila, wajoli walijikuta bila kitu chochote cha kujipatia riziki isipokuwa mili yao tu, isipokuwa uwezo wao wa kufanya kazi, nguvukazi. Kwa sababu hii, hawakuwa na budi ila kukimbilia mijini kuuza nguvukazi yao kwa viwanda vya mabepari. Ndiposa wakageuka kutoka kuwa wajoli wa kunyonywa na kunyanyaswa na makabaila na kuwa wafanyikazi ama *maproletarii* wa kumenyeka katika viwanda vya mabepari.

Nayo maisha ya wafanyikazi mijini yalikuwa maisha magumu mno. Yalikuwa maisha ya kinyama, ya kusaga meno, ya njaa na ukosefu, ya umaskini na wasiwasi, ya ufukara na sulubu. Yalikuwa maisha ya kufanya kazi kama watumwa katika hali hatari. Yalikuwa maisha ya kuishi katika "mathare" mijini, maisha yaliyokuwa mbali sana na uhuru na haki za binadamu. Haya ndiyo maisha walioishi wafanyikazi huko Ulaya Magharibi na hatimaye Urusi na popote pale ubepari ulipokuwa unajijenga na kujiimarisha.

Kwa upande wao mabepari waliendelea kupanua mitaji yao na kuzidisha utajiri wao kwa kuwanyonya na kuwagandamiza wafanyikazi. Kwani wakati wote harakati za kitabaka, mapambano kati ya wafanyikazi na mabepari, waajiriwa na waajiri, wanyonywaji na wanyonyaji, ni sehemu ya maisha ya kila siku katika ubepari tangu kale na zamani. *Na kila ongezeko, hata likiwa kidogo namna gani, la kidemokrasi, hutokana na mapambano makali ya wafanyikazi na wote wanaonyonywa na kugandamizwa.*

8.2. Uchambuzi wa demokrasi ya kibepari

Lenin

Mzalendo mkuu wa Urusi na dunia
mfano halisi wa mkomunisti
maana ya maisha ya mwanamapinduzi
shujaa na mpenzi wa wote wanaonyanyaswa
taa ya wapigania haki za binadamu
bingwa wa fikra na falsafa ya ukombozi
sogora wa hila na mbinu za mapambano ya wanaonyonywa
jemedari wa jeshi la haki la wafanyikazi
jazanda na isitiara ya mapenzi kati ya binadamu

Ewe Lenin
Vladmir Ilyich Lenin
hasidi mkuu wa wanyonyaji na wagandamizaji wote
kiboko cha ubepari na ubeberu
mfuasi msanifu na mkweli wa Marx na Engels
mfafanuzi mtetezi na mwendelezi wa usoshalisti

kinadharia
kiitikadi
kimatendo
na kiadili
unaesisitiza wakati wote
njia pekee na isiyoweza kuepukika
ya maendeleo na ukombozi wa wanaonyonywa
na hatimaye wa jamii kwa ujumla
ni njia ya ukomunisti;
Ndugu Vladmir
unaetufunza
umuhimu wa chama
chama cha kikomunisti
kilicho ngao na mkuki
wa wanaopigania usoshalisti
chama cha wanaokubaliana
na kuaminiana kiitikadi
chenye kuzingatia
demokrasi na nidhamu ya kimapinduzi
kinachozua mbinu na hila zake
kufungamana na nadharia ya upembuzi na uyakinifu
inayotushauri tunaopambana
tuchukue msimamo wa kitabaka kila mara
katika kutafsiri hali ya jamii
tukikumbuka wakati wote
umarx u hai na daima
unadai usanii na ubunifu
na ni kinyume kabisa cha ukasuku
tupambane pasina kurudi nyuma wala kukata tamaa
kwani gurudumu la historia
lingekuwa na mwendo wa upogoupogo
linazunguka mbele tu, daima mbele;

Oh Lenin
Vladmir Ilyich Lenin
ambae umewahi kuwa mfungwa wa kisiasa
baada ya kufukuzwa kutoka chuo kikuu
ulielazimika kuwa mkimbizi wa kisiasa katika enzi zako
huku niliko ninakukumbuka
daima nakupenda, tena sana
maisha yangu yakikaribia kuwa kama yako
lau hata kidogo tu
nikikukaribia Lenin mpendwa
nitajihesabu nimeishi;

Komredi Lenin
propaganda zote hizi wanazopropageti
hazitotufanya tuukumbatie ubeberu
kandamizo zote hizi wanazotukandamiza
hazitaweza kuusafisha mfumo mchafu wa ubepari
nyanyaso zote hizi wanazotunyanyasa

hazitaweza kuuokoa mfumo wa unyonyaji wa mtu kwa mtu
dhuluma zote hizi wanazotudhulumu
hazitawafanya wananchi waukubali udikteta
mateso haya yote wanayotutesa
hayatageuza ukweli kuwa uwongo na haki kuwa batili
usaliti huu wote wanaotusaliti wananchi wengi
hakika hatutouvumilia milele
kwani ewe ndugu yetu Lenin
jina lako
na majina ya wazalendo na wanamapinduzi
yako hai
na yatadumu na sisi milele
wanyonyaji wapende wasipende
sisi tunaowakumbuka
tunaopambania maisha mapya
tunaotafuta maendeleo na furaha ya wengi duniani
tunaokabiliana na majaribu tilatila
uliyokuwa ukikabiliana nayo
Lenin
Vladmir Ilyich Lenin
tuko nawe siku zote
wakitaka wameze wembe maadui wa ukomunisti popote walipo
bali jina lako komredi mpendwa Lenin
litadumu daima dawamu
mchango wako
kwa elimu na falsafa
kwa maendeleo ya binadamu
kwa harakati za ukombozi
hauna kifani
uliishi ndugu mpendwa uliishi
uliishi ipasavyo mtu kuishi
na kwa hivyo utaishi daima dawamu
nyota ya wanamapinduzi
Vladmir Ilyich Lenin.....

Mwandawiro Mghanga, Jela Kuu ya Kibos 6-2-1988

8.2.1. Umuhimu wa kuchambua demokrasi ya kibepari

Ni muhimu tujadiliane kuhusu demokrasi ya kibepari kwa kirefu. Hii ni kwa sababu *demokrasi ya kibepari ndiyo inayofikiriwa na Wakenya wengi kuwa kilele cha demokrasi. Propaganda za mabepari wa kimataifa kupitia kwa redio, televisheni, magazeti, sinema na vitabu nchini Kenya na kutoka nje zinakusudiwa kuonyesha ati demokrasi ya kibepari ndiyo mwanzo na ndiyo mwisho wa demokrasi na ati hapawezi kuwa na demokrasi yoyote ile duniani isipokuwa ya kibepari!*

Tunaelezwa usiku na mchana ati dola katika nchi za kibepari liko kwa ajili ya watu wote katika jamii na liko hapo ili kulinda maslahi ya kila mtu bila kujali anatoka tabaka gani. Ati dola halipendelei upande wowote ati linalinda maslahi ya jamii yote kwa ujumla. Hivyo, ati demokrasi katika ubepari ni serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa ajili ya watu. *Uongo* huu unatungwa makusudi kabisa na mabepari kwa kuwa katika nchi za kibepari demokrasi

inafanyia mabepari kazi kuu muhimu: kazi ya kupunguza migogoro, isiyoweza kuepukika, kati ya waajiri na waajiriwa, matajiri na maskini. *Demokrasi inalengwa kupoza ama kuzima harakati za kitabaka***.**

8.2.2. Demokrasi ya kibepari ni demokrasi ya mabepari

Ukweli unaoonekana wazi kila siku ni kwamba, kwa vyovyote vile, dola la ubepari linaongozwa na mabepari, na itikadi ya kibepari, na adili ya kibepari na liko hapo ili kuulinda mfumo wa ubepari na ubeberu. Mabepari wanaweza kuvumilia chochote kile bora tu kisiwe na nia na uwezo wa kuungasha mfumo wa ubepari. Upinzani ndani ya mfumo wa ubepari ni halali lakini ule wa kuuangusha ubepari ni haramu na hasidi. Dola katika nchi za kibepari ni mashini ya tabaka la mabepari ya kuwanyonya na kuwanyanyasa wafanyikazi na wale wote wasiyo na umilikaji wa viwanda, biashara kuu, mashamba makubwa na njia kuu za uzalishaji. Ni la kuwatawala na kuwagandamiza wale wanaoishi kwa kutegemea ujira, wavujajasho, wakodeshaji nyumba, wale ambao ni mafukara ama walalahoi. Ni kweli kuwa kihistoria, dola la kibepari ni la hali ya juu zaidi kwa wingi na ubora kulingana dola za hapo awali. Kwa ujanja wake, ambao ni pamoja na kujificha ndani ya demokrasi ya kibepari, dola la kibepari linaonekana kana kwamba liko kwa ajili ya taifa na kila raia pasina mapendeleo. Bali, chambilecho Lenin, jinsi linavyozidi kukomaa zaidi ndivyo linavyozidisha uwezo wake wa kuwakanganya na kuwanyanyasa watu wa tabaka la wafanyikazi na mafukara kwa ujumla.

Demokrasi ya kibepari, ni serikali ya mabepari inayoongozwa na mabepari kwa ajili ya mabepari na mabeberu. Msingi wa demokrasi ya kibepari ni mfumo wa ubepari, itikadi ya kibepari na dola la ubepari.

8.2.3. Demokrasi ya kibepari hupinga wanaopinga ubepari na ubeberu

Ndiyo kwa sababu USA, Ulaya Magharibi na nchi za kibeberu ulimwenguni, zinatangaza vita vya kisiasa, kiuchumi, kiitikadi, kidiplomasia na kijeshi dhidi ya taifa lolote lile ambalo linaenda kinyume cha maslahi ya ubepari na ubeberu.

Dola lolote ambalo linaongozwa na wazalendo, linalozingatia maslahi ya raia wake ama linalokataa mfumo wa ukolonimamboleo ama linalochagua kufuata barabara ya maendeleo ya kisoshalisti linapigwa vita baridi na moto dola za ubeberu wa kimataifa. Nchi za kibeberu, katika mfumo wa utandawazi[3] wa ubepari, hivi sasa zimejipa kazi ya kujenga taratibu mpya ya kimataifa, taratibu ya kufanya ulimwengu wote uwe chini ya makucha ya ubepari na ubeberu**.** Dola za kibepari zinafanya kazi ya kulinda makampuni hodhi ya kimataifa ya nchi zao ambayo yanazidi kutawala uchumi wa ulimwengu. Benki ya Ulimwengu, Shirika la Fedha la Kimataifa, Shirika la Biashara la Ulimwengu, na mikataba tilatila ya kimataifa na baina ya mataifa, zote ni taasisi zilizoundwa na dola za kibepari kuimarisha ubepari na ubeberu. Baada ya kuanguka kwa dola za 'kikomunisti' za Usoviet na Ulaya Mashariki, ubeberu unatawala ulimwengu vururumtende. Nchi zinazojulikana kama za ulimwengu wa tatu, zinazidi kupoteza uhuru wao wa kitaifa, uwezo wa kujiamulia sudi zao wenyewe, huku zikishindiliwa katika ufukara, kunyonywa, kubaki nyuma kwa maendeleo na kutegemea 'misada' ya mabeberu haohao! Isitoshe, mara nyingi haya yanafanywa kwa jina la kutetea demokrasi na haki za binadamu ulimwenguni! Lakini, je, dola ambazo zinatumika kulinda maslaha ya tabaka la wachache na kuwanyonya na kuwanyanyasa wengi nyumbani kwao kwenyewe, linawezaje kulinda na kutetea demokrasi na haki za binadamu za watu wa mataifa ya kigeni? Demokrasi inayozingatia falsafa

[3] Tutajadili kuhusu utandawazi katika makala mengine.

ya unyonyaji wa mtu kwa mtu inawezaje kuwa demokrasi ya watu wote katika jamii iliyogawanyika kitabaka?

8.2.4. Propaganda za demokrasi ya kibepari zimepenya Kenya

Nchi za kibepari zinatumia kila njia kujigamba kuhusu uhuru, demokrasi na haki za binadamu. Ndiyo kwa sababu itikadi ya vyama vya kisiasa na makundi mengi ya watu ambao hivi sasa wanapambana dhidi ya udikteta wa Moi-Kanu na kupigania demokrasi Kenya, ni itikadi ya kibepari. Wakenya wengi, hata wengine wakiwa wenye nia nzuri, wanajikuta wakipigania demokrasi ya kibepari kama lengo la msingi. Hata ukiwauliza wengi kuhusu maana ya demokrasi, watakuambia kuwa wanataka Kenya iwe kama USA, Wingereza, Canada, Ujerumani Magharibi, Ufaransa, Japan, n.k. Wanaamini ati demokrasi ya kibepari ndiyo Alfa na Omega ya demokrasi. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayodhaminiwa na nchi za kibeberu, yanafanyia kazi ubepari na ubeberu kueneza mawazo ya demokrasi ya kibepari miongoni mwa umma wa Kenya. MYK ya Kenya yanatumia nadharia ya kibepari kuhusu maendeleo, haki za binadamu, jinsia, mazingira, haki za kijamii, katiba, utawala, uwazi, uwajibikaji, n.k. Yanasaidia kuwarubuni Wakenya wengi wanaonyonywa na kugandamizwa ati wanaweza kujikomboa kutoka kwa imla na umaskini ndani ya mfumo wa ubepari na ukolonimamboleo. Vyama vya kisiasa vilivyoko bungeni hadi sasa vilevile vinasaidia ubepari na ubeberu kuendelea kukanganya umma na kupinga uhuru na ukombozi wa taifa letu huku vikiropoka na kupayuka bungeni na mikutanoni kuhusu demokrasi. Mabepari wa kienyeji, mabepariuchwara wa kila aina mkiwemo wataalamu na wasomi wa mlengo wa kulia, wanaikumbatia demokrasi ya kibepari kwa kuwa hiyo ndiyo inayoweza kuwahakikishia nafasi yao ya kujitajirisha na kufurahia maisha ya anasa na starehe kwa kuwanyonya na kuwatawala wengi ambao ni wafanyikazi, wakulima-makabwela, wenye kutegemea mishahara, wasiyo na kazi, maskwata, wanafunzi wengi, walalahoi, n.k. Dola la Kenya, linaloongozwa na vibaraka na wasaliti ni ngome ya ubepari na ubeberu.

8.2.5. Haki za binadamu chini ya demokrasi ya kibepari: kilemba cha ukoka

Demokrasi ya kibepari inawaahidi wananchi wote haki za kikatiba, kama usawa katika sheria, uhuru wa kusema na kusambaza maoni, uhuru wa kutembea na kujumuika, haki ya matibabu, haki ya kujipatia riziki, haki ya kuwa na nyumba bora, haki ya elimu kwa kila raia, haki ya kuchagua au kuchaguliwa kiongozi, n.k.

Lakini ikichunguzwa katika hali halisi ya maisha ya kila siku katika nchi za kibepari inaoneka kwamba kuna tofauti kubwa kati ya kukuwepo kwa haki za binadamu katika katiba na utekelezwaji wa haki hizo. Katiba ya kitaifa ya kibepari ni chombo kinachotumika kuwavisha vilemba vya ukoka wale wa tabaka zinazonyonywa na kunyanyaswa.

Msingi wa katiba za kibepari ni kulinda na kuabudu haki ya mtaji na mali ya binafsi. Kwa mfano, mabepari wana haki ya kuwa na mali ya binafsi na kuikuza kwa vyovyote vile hata kwa kuwanyonya na kuwanyanyasa wafanyikazi katika viwanda, makarakana, makampuni, na popote pale penye mitaji yao. Sheria nyingi ziko kwa ajili ya kulinda mali wanazochuma.

Nao wafanyikazi na wananchi wa tabaka lisilo na umilikaji wa njia kuu za uzalishaji, wanahakikishiwa na katiba haki ya kuwa mabepari wakitaka. Lakini, utake usitake bila mtaji huwezi kuwa bepari. Huwezi kutoka kwa tabaka la wafanyikazi na kuingia tabaka la mabepari ati kwa kuwa umeamua tu kufanya hivyo na au kwa sababu unaruhusiwa na katiba. Fauka ya haya kuna vikwazo tilatila katika jamii za kibepari vya kuhakikisha kuwa uwezo wa mtu kutoka tabaka la wafanyikazi kuingia katika tabaka la mabepari ni sawa na ule wa ngamia kupitia tundu

la sindano. Ndiyo kwa maana, katika nchi za kibepari, jamaa za matajiri ni zilezile za kutoka kale na zamani. Aidha, pengo kati ya matajiri na maskini linazidi kupanuka, matajiri wanatajirika zaidi huku maskini wanafukarika zaidi. Hayo madai ya watetezi wa mfumo wa ubepari ati mtu yoyote katika jamii hiyo akijitahidi kwa uwezo wake wote anaweza kuhama tabaka la mafukara hadi tabaka la mamilionea ni porojo za kuwakanganya wanaodhulumiwa kwa kuwapa matumaini ya bure. Chimbuko cha umaskini si kuwa maskini hawafanyi kazi au bidii bali ni mfumo unaohakikisha kuwa kazi na bidii ya maskini inamfaidi tajiri badala ya yeye mwenyewe. Asili ya utajiri wa tajiri si kazi na bidii ya tajiri bali ni umilikaji wa njia ya uzalishaji inayomwezesha kuwanyonya wafanyikazi. Ndiyo kwa maana, ndoto ya Marekani, ambapo inadaiwa ati mtu akiingia Marekani tu atapata fursa ya kuuhama umaskini na kutajirika, imebaki ndoto tu isipokuwa kwa matajiri.

8.2.6. Je haki ya kila mtu kuwa na kazi inatekelezwa?

Chini ya demokrasi ya kibepari, wafanyikazi wanahakikishiwa haki ya kikatiba ya kufanya kazi wanayoitaka pahali wanapotaka na kupigania kulipwa ujira wanaoutaka. Bali hili haliwezi kutekelezwa katika hali ambapo ukosefu wa kazi hivi sasa unazidi kuwa donda ndugu katika nchi za kibepari. Ubepari wa ukiritimba na utandawazi wa kibeberu unaathiri vibaya mno wafanyikazi katika nchi za kibepari. Kutokana na maendeleo ya haraka ya sayansi na tekinolojia, hasa katika nyanja za usambazaji wa habari, kompyuta na usafiri, mtaji unazunguka ulimwenguni kwa urahisi na kasi mno. Mabepari wanatoa vitegauchumi vyao kutoka kwa mataifa yao ambapo kanuni juu ya ushuru, haki za wafanyikazi, mazingira, n.k. inawazuia kuchuma faida wanayoitaka. Badala yake wanaweka vitegauchumi vyao pahali pengine ulimwenguni wanapoweza kukwepa kanuni hizo na kuchuma faida nyingi na kwa haraka zaidi. Ndiyo kwa maana wakati makampuni madogo yanafilisika au kuungana na makampuni makubwa zaidi huku yakizidisha ukiritimba wa ubepari ukitia fora, kupanuka kwao ulimwenguni kunamaanisha kufutwa kwa wafanyikazi nchini mwao.

Isitoshe, katika enzi za utandawazi wa ubeberu, mtaji wa pesa badala ya mtaji halisi wa uzalishaji mali, ndiyo unaowapa mabepari faida kubwa na ya haraka zaidi hasa kwa kuwa mabilioni kwa mabilioni ya pesa yanazunguka ulimwenguni kila siku kwa njia ya mtandao wa intaneti. Bali ni mtaji halisi wa kuongeza uzalishaji mali katika ardhi na viwanda ambao huongeza ajira.

Fauka ya haya, ni kanuni ya ubepari kuwa wakati maendeleo ya sayansi na tekinolojia yanazidisha faida na mtaji wa mabepari, wakati huo huo sawia yanazidisha ukosefu wa kazi na kunyonywa kwa wafanyikazi na mabepari. Leo katika nchi za kibepari, pengo kati ya matajiri wachache na wengi kutoka kwa tabaka la wafanyikazi linazidi kupanuka. Umaskini unaongezeka usiku na mchana. Nazo harakati za kitabaka zinazidi kutokota na kuchemka. Katika hali hii, kuzungumza kuhusu haki ya kuajiriwa kazi kuna maana gani?

8.2.7. Haki na sheria ni bidhaa chini ya ubepari

Je ni kweli kuwa kuna usawa mbele ya sheria kwa wananchi wote katika nchi za kibepari kama demokrasi ya kibepari inavyodai? La, kama tulivyosema hapo awali, *matajiri na maskini kamwe hawawezi kuwa sawa.* Haki katika nchi za kibepari inauzwa kama bidhaa yoyote ile sokoni. Ukiwa na pesa una uwezo wa kuajiri wakili bora na unaemtaka kukutetea mahakamani, uwe umekosa ama la. Unaweza hata kujiokoa kwa kuwahonga mahakimu. Bali ukiwa maskini, ni muhali kupata huduma za wakili na kwa hivyo huna haki sawa na tajiri katika mahakama.

Isitoshe, mfumo wa ubepari ni mfumo wa unyonyaji wa mtu kwa mtu. Kuwanyonya wafanyikazi ama watu wowote wale ni halali kabisa kufungamana na sheria na adili za kibepari. Kujitajirisha kwa kutumia jasho la watu wengine si kuvunja sheria au haki za binadamu katika ubepari! Lakini kwa maskini kumnyonya tajiri ni kosa linaloitwa wizi au unyang'anyi.

Katika nchi za kibepari, zikiongozwa na Marekani, mafukara na wengi wasio na njia halali ya kujipatia riziki, wamejaa magerezani kwa kulazimika kufanya uhalifu ili waishi. Kwa kutaka kujiokoa ama kuukimbia umaskini kwa njia hiyo, wanatisha mali ya binafsi. Ndiyo kwa maana magereza yamejengewa watu wa tabaka la maskini. Kwani hata wengi wa viongozi wanaopatikana na hatia za ufisadi kila siku katika nchi za kibepari, hawachukuliwi hatia za kuhukumiwa vifungo virefu ama kulazimishwa kurudisha mali za umma walizozipora. Mara nyingi, watu wakilalamika sana wezi wakuu kutoka kwa tabaka tawala wanalazimishwa kujiuzulu na mamilioni waliyoyaiba.

Yanayoendelea hapa kwetu nyumbani ambapo viongozi wanaiba mabilioni na kuendelea kuwa huru na viongozi wakati ambapo mafukara wananyongwa kwa kuiba shilingi mia moja, ni sehemu ya demokrasi ya kibepari. Viongozi wakiiba, wakipora mali ya umma ama wakivunja sheria kunatungwa tume za uchunguzi. Hizo tume zinatumia pesa nyingi sana na hatimaye wanaokuwa mamilionea kwa kufilisi mashirika ya umma ama kwa kuibia serikali hawapatikani na hatia yoyote au hawafunguliwi mashtaka. Lakini maskini akiiba hata shilingi moja anaitiwa polisi mara moja na kupelekwa mahakamani ambapo anahukumiwa kufungwa jela au hata kunyongwa. Hukumu za kufungwa na magereza ni kwa ajili ya mafukara wa duniani. Hii ndiyo haki ya ubepari.

8.2.8. Matajiri wana huduma za matibabu bora zaidi kuliko maskini

Ingawa demokrasi ya kibepari inadai kuwa inawapa raia wake wote haki za matibabu, ukweli halisi ni kwamba matajiri ndiyo wanaotekeleza haki hii mara nyingi zaidi kuliko maskini ama watu wasio na mali. Ukiwa na pesa utaweza kula vizuri zaidi, kuwa na nyumba bora zaidi, kuvaa vizuri zaidi, kukaa katika mazingira mazuri zaidi na kuishi vizuri kwa kila hali kuliko watu wa kawaida. Aidha, utaweza kununua huduma bora zaidi za madaktari, hospitali na matibabu kuliko makabwela. Kwani katika nchi za kibepari, udaktari, mahosipitali na matibabu ni biashara pia kama biashara yoyote ile inayowatajirisha watu binafsi kwa kuwanyonya wagonjwa. Adili za udaktari, ambazo ni pamoja na kujitahidi wakati wowote kuokoa maisha, hazitekelezwi katika mfumo unaoonguzwa na adili ya kuchuma mali kwa vyovyote vile. Udaktari kama utaalamu wowote ule unatumika kama njia ya kushiriki katika unyonyaji uliyoko katika jamii.

8.2.9. Matajiri wana fursa zaidi ya kujiendeleza

Inadaiwa ati chini ya demokrasi ya kibepari kila mwananchi anatekeleza haki ya kupata elimu kiasi cha uwezo wake. Ati kila raia ana fursa sawa ya kujieneleza na kupanua vipawa vyake. Huu pia ni uongo mwingine. Kwani inajulikana kwamba katika nchi za kibepari elimu ni bidhaa kama bidhaa yoyote ile. Wenye hela wanaweza kununua elimu nyingi na bora zaidi. Ndiyo kwa sababu watoto wa matajiri wanasoma katika mashule na makoleji bora zaidi kuliko wale wa watu wa kawaida. Nayo hayo mashule ya watoto wa matajiri yana walimu bora zaidi, vifaa bora zaidi na mazingira bora zaidi ya elimu kuliko yale ya watoto wa makabwela.

Huwezi kabisa kuthibitisha ati watu wote wana nafasi sawa za elimu katika ubepari. Ndiyo kwa sababu, migomo ya wanafunzi ni sehemu ya maisha ya kila siku katika Ufaransa, Korea Kusini, USA, Wingereza, n.k. ambapo wanafunzi wanapinga njama za serikali zao za kuwapora haki chache za elimu na uhuru wa kiakademia ambazo zilipatikana kutokana na mapambano

makali. Polisi wanatumiwa kupambana dhidi ya wanafunzi wanaoandamana na kukutana kupinga maongozi ya kibepari ya serikali za nchi zao ambayo kila siku yanasababisha ukosefu wa kazi, kuongezeka kwa tatizo la nyumba, inflesheni, kupungua kwa huduma za jamii, mkiwemo elimu kwa wananchi wengi.

8.3. Tajiri anatekeleza haki ya kusema zaidi kuliko maskini

Ndiyo, tunaambiwa ati kila raia katika nchi za kibepari ana haki ya kusema na kusambaza maoni yake bila hofu yoyote ile. Bali mabepari ambao wanamiliki magazeti, maredio, matelevisheni na majumba ya kuchapisha vitabu wanatekeleza haki ya kusema na kusambaza maoni yao zaidi kuliko wananchi wengi wa kawaida. Wanasikika kwa watu wengi zaidi. *Ndiposa itikadi ya kibepari ndiyo inayotawala katika nchi za kibepari, kwani inasambazwa kwa watu wengi zaidi kila siku.*

.

Maana ya kampeni za wanasiasa za ubunge au vyama, hakika ni utumiaji wa vyombo vya habari kuwakanganya wananchi na kuwanywesha propaganda za ahadi za uongo na kweli. Uhuru wa vyombo vya mawasiliano katika nchi za kibepari, ni uhuru wa mabepari wa kusambaza maoni yao jinsi wanavyotaka, kwani idadi kubwa zaidi ya vyombo vya mawasiliano katika nchi za kibepari vinadhibitiwa na mabepari wenyewe.

Magazeti ya siasa za mlengo wa kushoto ni machache mno, ni maskini sana kulingana na yale ya siasa za mlengo wa kulia na yanapigwa vita baridi na mara nyingine moto na dola la ubepari.

Isitoshe, hata ingawa una haki ya kikatiba ya kusema na kusambaza maoni yako, kuna hatari kwamba ukimkasirisha mwajiri wako kwa maoni yako unaweza kukosa nafasi ya kupandishwa cheo au hata ukapigwa kalamu kabisa. Wahariri na waandishi wa magazeti, kwa mfano, sharti wazingatie sera za uhariri za magazeti yao ambazo zinatungwa na mabepari, waajiri wao. Katika vyuo vikuu vya nchi za kibepari, wasomi na walimu wenye mitazamo ya kikomunisti wananyanyaswa kwa njia mbalimbali. Ni muhali kudhaminiwa kufanya utafiti wa maswala mbalimbali ya jamii ikiwa unatumia nadharia ya kikomunisti.

Maoni ya raia yatavumiliwa na dola la ubepari kadiri ambapo yataendelea kuwa katika mipaka iliyowekwa na mabepari wenyewe. Yakiwa ni malalamiko matupu, yakiwa ni kelele za chura ambazo haziwezi kumzuia ng'ombe kuendelea kunywa maji, yakiwa ni mawazo ya kupigania marekebisho ndani ya mfumo wa ubepari ama ya kuwasilisha itikadi ya kibepari kwa maneno mengine yaliyo tofauti na ya serikali iliyoko, hapo angalawa yatavumiliwa.

Hata maoni ya kupigania kuvunjwa kwa mfumo wa kibepari yanaweza kuvumiliwa ikiwa yatafikia watu wachache iwezekanavyo na pasina taratibu madhubuti ya kupigania malengo hayo. Ndiyo kwa maana magazeti ya vyama vya mlengo wa kushoto, mkiwemo vya kikomunisti, yanakubaliwa katika nchi za kibepari. Lakini mawazo ya kikomunisti yakianza kutoka kwa chama cha kikomunisti na kuwafikia mamilioni ya umma wa wafanyikazi, hapo dola la kibepari litaanza kutumia njia za kila aina kuyazuia, hata njia za kiharamia. *Kukuwepo kwa vyama vya kikomunisti katika nchi za kibepari, kunatokana na historia ndefu ya mapambano makali ya wafanyikazi na wakomunisti.* Na vita vya kila siku wanavyopigwa wakomunisti kwa kila hali na vyombo vya dola si haba.

Nchini Ujerumani, kwa mfano, kuna sheria inayosema kwamba mtu yoyote yule ambae hakubaliani na katiba ya kitaifa hawezi kuajiriwa kazi ya serikali. Na kwa sababu katiba ya Ujerumani ni ya kibepari, wakomunisti au watu wanaojitambulisha na ukomomunisti, hawaajiriwi kazi za uwalimu, afisi za serikali, ubalozi, n.k. Kutumia sheria hii, baada ya Ujerumani Magharibi

kuungana na Ujerumani Mashariki kuna maana kuwa raia wa kutoka Ujerumani Mashariki wakiwemo walimu, wasomi, wanasayansi, wanajeshi, wataalamu wa kila aina, maafisa wa zamani wa dola la Ujerumani Mashariki, hivi sasa wamejikuta bila kazi wala hawana matumaini ya kuajiriwa ati kwa sababu walikuwa wakomunisti ama wakitumikia dola la ukomunisti. Wakati huohuo, sawia, tunaambiwa kuwa Ujerumani ni mfano wa demokrasi wa kuigwa na sisi!

9. Mizani ya demokrasi yoyote ile ni utekelezaji wake

Tunaweza kutoa mifano mingi kuonyesha uhange na unafiki wa demokrasi ya kibepri. Kwa sasa inatosha tu kusisitiza kwamba *mizani ya demokrasi ycyote ile ni utekelezaji wake*. Haitoshi tu kuahidi wananchi haki nyingi iwezekanavyo katika katiba ikiwa hawazifaidi kutokana na utekelezaji wake katika maisha ya kila siku. Katiba ikiahidi kuchunga haki ya maisha ya kila raia basi lazima kukuwepo na mpango halisi utakaowawezesha wananchi kuwa na kazi ama njia ya kujipatia riziki, kula chakula bora, kuvaa nguo za kutosha na bora, kuishi kwa nyumba za kufaa, kupata matibabu wakiwa wagonjwa, kunufaika na elimu, n.k. Kumwambia mtu asie na nyumba wala makao kuwa katiba inalinda uhuru wake wa kutoingiliwa na kusumbuliwa na polisi ama mtu yoyote katika nyumba yake, ni kumpaka mafuta nyuma ya chupa raia huyo. *Demokrasi ya kibepari inatia fora katika kuwavisha vilemba vya ukoka wananchi wengi, hasa wa tabaka linalonyonywa na kunyanyaswa. Lengo lake ni kupoza harakati za kitabaka.*

Ni muhimu sana kuzingatia ukweli huu hasa wakati Wakenya wanadanganywa ati suluhisho la matatizo tilatila yanayokumba nchi yetu ni kuwa na katika mpya ya kitaifa. Bila haya, shirika moja lisilo la kiserikali linalodhaminiwa na mabeberu linasambaza maandishi yanayosema, ”Katiba Mpya Maisha Mapya”! Huu ni uongo mtupu. Katiba mpya inaweza kuwa ngazi ya kupambania maisha mapya ikiwa inasimamia maisha mapya na itatekelezwa ipasavyo. Lakini hata iwe katiba ya kidemokrasi kiasi gani, ikiwa bado kuna mfumo wa ubepari, hapawezi kuwa na maisha mapya kwa watu wa tabaka la wengi, wakulima na wafanyikazi. Maisha mapya na bora kwa wengi yataletwa na mfumo wa kisoshalisti.

10. Umbo la demokrasi ya kibepari

Umbo la demokrasi ya kibepari halifanani katika kila nchi. Katika nchi zingine, kama USA na Ufaransa kwa mfano, wana mtindo wa uraisi ambapo raisi anachaguliwa na wananchi na anakuwa na uwezo wa kuunda serikali. Katika nchi hizi, raisi ana uwezo mkubwa sana kufungamana na katiba.

Pahali pengine, kama Wingereza, Japan ama Sweden, wanafuata mtindo ambapo chama kinachoshinda viti vingi vya kibunge kinaunda serikali ambayo inasimamiwa na waziri mkuu. Waziri mkuu anawajibika kwa bunge. Naye mfalme au malkia ndie anaekuwa mkuu wa dola, ijapokuwa kijazanda tu.

Jinsi kura zinavyopigwa na taratibu zinazofuatwa katika kuwachagua viongozi wa serikali kuu na serikali za majimbo ama mitaa, ni tofauti katika kila nchi. Taasisi za kidemokrasi hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Hata hivyo, *katika nchi za kibepari, matajiri, mamilionea ama watu kutoka kwa tabaka la mabepari, ama wenye uhusiano halisi na wenye kuhodhi viwanda, makampuni makubwa, mashamba ya kibepari, na wamilikaji wa uchumi mkuu wa kitaifa, ndiyo huchaguliwa kuongoza serikali za kibepari karibu kila mara na katika nchi zote za kibepari.*

Umbo lingine la demokrasi ya kibepari ni *mfumo wa vyama vingi vya kisiasa*. Bunge na mfumo wa vyama vingi vya kisiasa ni kilele cha demokrasi ya kibepari. Hata hivyo, mfumo wa vyama

vingi vya kisiasa unatokana na kutambua kukuwepo kwa tofauti za kitabaka na kimakundi. Ni juhudi za kujaribu kuficha au kupoza harakati za kitabaka. Kwani mfumo wa vyama vingi, aidha, hutumiwa na mabepari kuwadanganya wananchi kuwa watu wote katika jamii wana haki sawa za kidemokrasi. Kura zinazopigwa kila baada ya miaka mitatu, minne au mitano, huwafanya wananchi wengi wanaonyonywa kutarajia serikali mpya na mabadiliko ya kuboresha maisha yao ndani ya mfumo wa ubepari.

Bali *kinachoweza kubadilika chini ya ubepari, labda ni sura za viongozi tu lakini dola hubaki dola lilelile la kibepari na mfumo hubaki huohuo wa ubepari na taasisi zilezile za kibepari na itikadi ileile ya kibepari*. Kwani mara nyingi vyama vikubwa zaidi, vyenye fedha zaidi, vyenye sauti zaidi ni vya mkondo mmoja ama mwingine wa ubepari.

Kwa mfano, huko USA, kuna vyama viwili vikuu ambavyo hupigania uongozi wa nchi hiyo, Republicans na Democrats. Wakati wa kampeni, vyombo vya habari hutumiwa kuonyesha kwamba chama kimoja kikishinda kutakuwa na mabadiliko makubwa sana ya ndani na ya nje ya nchi hiyo. Bali kila mara wananchi wa USA na dunia hugundua kuwa maongozi ni yale yale tu, ya kibepari na kibeberu. Kinachobadilika ni sura za watu tu bungeni na serikalini zikiandamana na marekebisho machache hapa na pale ndani ya nchi hiyo. *Bali siasa ya ndani na nchi ya nje ya USA, kimsingi, haibadiliki. Huwa ni ileile ya kibepari na kibeberu, wawe Republicans wawe Democrats.* Hii vilevile ndiyo hali iliyoko katika nchi zote za kibepari na kibeberu.

11. Vyama vya Demokrasi ya Kijamii

Pamoja na vyama vya kibepari vya kila aina, katika nchi za kibepari vilevile kuna vyama vya Demokrasi ya Kijamii (Social Democratic Parties) na vyama vya kikomunisti. Vyama vya Demokrasi ya Kijamii bado vina wafuasi wengi kutoka kwa tabaka la wafanyikazi na wakulima kwani vina historia yake katika tabaka la wafanyikazi na mapambano ya wafanyikazi dhidi ya ubepari. Lakini vimeingiliwa, kuparaganywa na kumezwa na siasa za itikadi ya kibepari na uongozi wa kisabili na kibarakala wa mabepari-uchwara.

Vyama vya Demokrasi ya Kijamii vimeasi misingi ya itikadi ya kisoshalsti, hasa kuhusu swala la dola na harakati za kitabaka. Vimeshikilia siasa za kujaribu kuandika upya nadharia ya usoshalisti wa kisayansi ili iambatane na mawazo yao ya kisabili na kibepari. Badala ya kupigania mapinduzi ya kuuvunijilia kabisa na milele mfumo wa ubepari, demokrasi ya kijamii inapigania maisha bora kwa wanaonyanyaswa ndani ya ubepari. Viongozi wa vyama vya demokrasi ya kijamii wanadanganya kuwa mfumo wa ubepari unaweza kuboreshwa na kufanywa kuwa wa kiutu. Wanahubiri kuwa ati kwa kupitia taratibu za ubunge na demokrasi ya kibepari wanaonyonywa na kunyanyaswa watajikomboa na kuwa huru. Wanakataa kuzingatia kuwa uhuru hauwezi kupatikana chini ya mfumo wenye mizizi katika falasafa na mahusiano ya kiuchumi ya kinyonyaji. Kwa sababu hii, vyama vya demokrasi ya kijamii si tisho kwa wenye kutawala uchumi na dola, mabepari, na kwa hivyo hukubaliwa hata kukamata hatamu za serikali mara kwa mara.

Wakati mwingine vyama vya demokrasi ya kijamii vikichukua serikali hufanya marekebisho kadhaa yanayoboresha maisha ya wafanyikazi na wananchi wengi kwa ujumla vikilinganishwa na vyama vya kibepari. Hali hii imekuwepo Sweden, Norway, Finland na Denmark, kwa mfano, ambapo wameweza kuwahakikishia wananchi wote, chakula bora, nyumba za kufaa, nguo, huduma za matibabu na elimu, pensheni kwa kila mwananchi, n.k. *Bali lazima tusisitize kuwa haya yote yametokana na mapambano ya wafanyikazi ya muda mrefu*.

Isitoshe, kadiri siasa za mlengo wa kulia zinavyozidi kujitoma katika nchi hizi, na kadiri ambapo uchumi wa kibepari unayumbayumba na kuzama, na baada ya kuangushwa kwa utawala wa kikomunisti huko Urusi na Ulaya Magharibi, huduma hizi za kijamii nazo zinakatwa usiku na mchana. Hivi leo siasa za ufashisti zinazidi kukua na kutisha demokrasi ya kibepari yenyewe. Usiku na mchana vyama vya demokrasi ya kijamii vinazidi kujitenga zaidi na siasa za kuwakilisha maslahi ya wafanyikazi na wanaonyonywa. Sera zao za kiuchumi na kisiasa za hivi leo hazina tofauti zozote za kimsingi na zile za vyama vya kibepari. Wafanyikazi na watu wa tabaka la wengi wanazidi kupoteza imani kwa siasa za demokrasi ya kijamii.

12. Vyama vya kikomunisti katika nchi za kibepari

Vyama vya kikomunisti vina lengo la kufanya mapinduzi, kuuangusha mfumo wa kibepari na kujenga mfumo wa kisoshalisti badala yake. Kwa hivyo, *vyama vya kikomunisti ni adui wakuu wa mabepari na vinapigwa vita baridi na moto mbele na nyuma kila siku.* Wakomunisti wanafanya kazi katika mazingira magumu mno, chini ya dola la hali ya juu la ubepari lenye uzoefu wa propaganda na katika jamii inayoleweshwa kasumba ya uzuri wa demokrasi ya kibepari na "hatari ya udikteta wa kikomunisti". Hali ya kwamba tabaka la wafanyikazi na mafukara katika nchi za kibepari linarushiwa makombo ya mabilioni kwa mabilioni ya pesa na mali yanayoporwa nchi zilizoko chini ya ukoloni-mkongwe na ukoloni-mamboleo inawafanya wafanyikazi wengi, kwa sasa, wanaswe katika mtego wa mabepari wa kuwafanya wajiepushe na "siasa kali kupindukia" za kikomunisti.

Hata hivyo, udhaifu mkubwa zaidi wa vyama vingi vikuu vya kikomunisti vya Ulaya Magharibi na katika nchi za kibepari, ni kuendelea kung'ang'ania nadharia potofu ya Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Wakomunisti (*Second International*). Nadharia ya Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Wakomunisti ambayo imechambuliwa na Lenin na wakomunisti wengine kwa marefu na mapana, na ambayo iliongozwa na Karl Kautsky – kigeugeu wa Austria, inahubiri kuhusu "ukomunisti" wa uongo: 'ukomunisti' wa kuparaganya misingi ya nadharia ya ukomunisti iliyowekwa na Karl Marx na Fredrick Engels na kuendelezwa na Vladmir Lenin; 'ukomunisti' wa kukana harakati za kitabaka; 'ukomunisti' wa kuabudu demokrasi ya kibepari na kupinga demokrasi wengi wanaonyonywa-udikteta wa wafanyikazi; 'ukomunisti' wa ubarakala na taasubi ya utaifa; 'ukomunisti' wa kuurekebisha ubepari badala ya mapinduzi ya kuuvunjilia mbali ubepari; 'ukomunisti' wa kupinga mbinu ya kutumia vita dhidi ubepari, 'ukomunisti' wa kutozingatia umuhimu wa chama halisi cha kikomunisti na jukumu lake la kuwa katika msitari wa mbele wa mapambano ya wafanyikazi na wote wanaonyonywa ya kunyakua nguvu za dola.

Kutokana na udhaifu huu, vyama vingi vikuu vya kikomunisti vya nchi za kibepari vina upungufu wa kusanii mbinu na hila za kuendesha propaganda za kikomunisti miongoni mwa wafanyikazi, vijana na wananchi kwa ujumla. Vimeganda katika njia za kikatiba za kupigania usoshalisti na zina upungufu wa programu za kuonyesha umuhimu na namna ya kunyakua nguvu za dola kutoka kwa mabepari.

Bali, wakomunisti katika nchi za kibepari wanafanya kazi kubwa kila siku ya kutetea demokrasi ya kibepari ambayo imeletwa na mapambano ya muda mrefu ya wafanyikazi, na ambayo daima inatishwa na mabepari na mafashisti. Wakomunisti wanasaidia kufichua uongo wa propaganda za mabepari, ufisadi na kuwaunga mkono watu wanaopambana dhidi ya udikteta, ubaguzi wa rangi, ukoloni na ukoloni-mamboleo duniani. Pili, pamoja na mambo mengine, wanajitahidi kufundisha kuwa kuna maisha mengine bora zaidi, ya hali ya juu zaidi, ya kiutu na kiadili zaidi kuliko yaliyoko katika mfumo wa ubepari. Hivi sasa wakomunisti wako katika msitari wa mbele wa kuongoza mshikamano wa umma wa ulimwenguni dhidi ya ubeberi kwa jina la utandawazi. Fauka ya hayo, vyama halisi vya kikomunisti, vinavyozingatia misingi ya kinadharia na kiitikadi

ya ukomunisti kwa maneno na vitendo, vinazidi kujengwa kila pahali katika nchi za kibepari. Mfano ni mikutano ya kimataifa ya vyama vya kikomunisti ya kila mwaka inayoandaliwa na Chama cha Wanyafikazi cha Ubelegiji (Workers' Party of Belgium).

13. Demokrasi ya kibepari: silaha ya ubeberu

Unafiki wa demokrasi ya kibepari unajidhihirisha zaidi katika siasa za nchi za nje za dola za nchi za kibepari. Wakati Wafaransa, mathalani, walipokuwa wakijivunia mapinduzi ya kibepari yaliyoleta demokrasi ya kibepari ikiwa na mwito wa uhuru, usawa na undugu, wakati huo huo sawia, walikuwa wakijaribu kudhibiti dola la kinyama la utumwa huko Haiti!

Wananchi wa nchi za Ulaya Magharibi walipokuwa wakifurahia haki za binadamu zilizoko katika katiba za nchi za kibepari, katika Afrika, Asia na Amerika ya Kilatino tumekuwa chini ya ukoloni wa nchi zao. Na *ukoloni ni kinyume kabisa na demokrasi na haki za binadamu.* Ufashisti waliyokuwa wakiupinga huko Ulaya, ulikuwa ukitendwa na nchi zao katika mataifa yaliyokuwa chini ya ukoloni kote ulimwenguni. Na wazalendo walipochukua silaha kuupinga ukoloni na ufashisti wake, kama sisi Wakenya na hatimaye watu wa Algeria, Msumbiji, Angola, Guinea Bissau, Zimbabwe, Namibia na Afrika Kusini, tumekuwa tukiitwa magaidi na washenzi wanaovunja haki za binadamu na demokrasi.

Ni nchi za kibepari zinazojivunia demokrasi na haki za binadamu ambazo zimekuwa zikiunga mkono kwa kila hali serikali ya makaburu wa Afrika Kusini na kuisaidia kupambana dhidi ya wazalendo wanaopigania demokrasi na ukombozi wa kitaifa. Sera ya serikali ya kibeberu ya USA ya kusaidia wasaliti na madikteta wa Amerika Kusini, Korea Kusini, Ufilipino, Israel, Uturuki na Amerika ya Kati na Afrika, kuendelea kuwanyonya, kuwagandamiza, kuwakanyaga na kuwawua raia wao, inajulikana wazi. Kwa jina la demokrasi na haki za binadamu USA ilivamia Grenada na kuendesha ufashisti wa ajabu huko Vietnum. Kwa jina la uhuru na demokrasi, USA na waitifaki wake wametangaza vita vya kiuchumi, kidplomasia, kisaikolojia, na kijeshi dhidi ya mataifa ya Cuba, Libya, Korea Kaskazini na Iraq. Kwa jina la demokrasi, nchi za kibeberu zimevunja taifa la Yugoslavia na kusababisha vita vya kinyama vya kikabila. Kwa jina la demokrasi Ufaransa imekuwa ikitumia nguvu za kijeshi kupinga mageuzi ya kizalendo huko Visiwa vya Ngazija, Jamhuri Afrika ya Kati, Kongo, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda, Burundi, n.k.

Kwa jina la demokrasi na haki za binadamu usoshalisti umeangushwa huko Urusi na Ulaya Mashariki na hivi sasa dola liko mikononi mwa mabepari, vibaraka wa mabeberu na magenge ya mafia. Matokeo yake ni kwamba mataifa haya ambayo yalikuwa huru na yakipiga hatua mbele kwa kila hali, hivi sasa yamekuwa mataifa ya kuomba na kusaidiwa, kunyonywa na kudharauliwa na ambayo kila siku yanadidimizwa katika umaskini, ushenzi, unyama na vita vya kikabila.

Umoja wa Mataifa umekuwa chombo cha nchi za kibeberu cha kulinda na kuendeleza ubeberu kwa kisingizio cha upolisi wa kimataifa wa kutetea haki za binadamu na demokrasi. Kwa kutumia taasisi za ubeberu kama Benki ya Ulimwengu, Shirika la Fedha la Kimataifa, Shirika la Biashara la Ulimwengu na mfumo wa utandawazi wa kibepari, nchi za kibeberu zinazishindilia nchi za Afrika, Asia na Amerika Kusini katika lindi la madeni yasiyoweza kulipika, kunyonywa na kufukarishwa, umaskini, njaa, inflesheni, ghasia, vita na matatizo tilatila ambayo yanawanufaisha tu mabepari vibaraka wao.

Kwa maneno mengine, kila anaeshiriki katika harakati za ukombozi wa kijamii na kitaifa, sharti atahadhari na njama za ubeberu.

Harakati za Kidemokrasi Kenya

Mau Mau

Wakulima na wafanyikazi wa nchi yetu
Waliukataa ukoloni-mkongwe
Waliugomea kwa maneno na kwa vitendo
Wakasema hapana!
Hapana kwa utawala wa watu weupe Kenya
Wakajizatiti usiku na mchana
Wakakutana wakafanya njama wakapanga mbinu na hila
Wakalishana viapo
Wakakula kiapo cha Kenya na uhuru wake
Wakaapa kujitoa mhanga kwa heri ama kwa shari
Kwa ajili ya ukombozi wa taifa letu
Wakakubaliana watapigana pasina kusita wala kurudi nyuma
Watapambana hadi watakapoukwamua ukoloni nchini
Kibirikizi kikalia
Mbiu ya mgambo ikatangaza vita vya ukombozi
Wanaume wakajitokeza
Wanawake wakajitoma mbele
Na watoto wasikubali kuwachwa nyuma
Hata wazee na wagonjwa wakawa tayari kutoa mchango wao
Hakukuwako mzalendo yoyote
Alietoroka mapambano ya uhuru
Kila aliejihesabu mzalendo alitoka kufanya sehemu yake
Wakulima na wafanyikazi
Wakaitikia mwito
Wakajitoa kwa ajili ya taifa letu
Wakasambaa mijini
Wakajitoma mashambani
Wakaingia misituni
Kwa mabunduki na mabomubomu
Kwa mapanga na magurunedi
Wakatangaza vita vya kigorila
Dunia nzima ikasikia ikapata habari
Kuhusu vita vya ukombozi vya Wakenya
Wakafahamu Wakenya wamefikia hatua ya kudai uhuru
Kuudai kwa mitutu ya bunduki
Jeshi la Uhuru na Mashamba likawa limeundwa
Sifa za Mau Mau zikasambaa kama upepo
Wana halisi wa Afrika wakawa kitu kimoja
Kupigania heshima ya mtu mweusi
Magogo wa mashujaa wa Kenya yetu
Wakawa wanazaliwa kila siku katika uwanja wa vita
Majemedari wa kwanza wa taifa letu
Wakawa wanaonekana wazi katika msitari wa mbele
Wazalendo wakawa upande huu
Na wasaliti wakakimbilia upande ule
Ndipo maana ya uzalendo na usaliti

Ikaeleweka bayana katika harakati za ukombozi wa kitaifa
Utamaduni wa kupambana dhidi ya ubeberu
Ukazidi kuota kukua na kunawiri kila pahali
Nyimbo za kuupinga ukoloni zikatungwa
Ngoma za kuimba uzuri wa uafrika zikacharazwa na kuchezwa
Fasihi ya kusimulia maovu ya kutawalwa na wageni ikatapakaa
Adili ya matumaini ya ushindi wa vita vyetu vya haki
Ikawa inasambazwa kwa wote hata maadui
Vita vya uhuru wa Mwafrika vikawa vinapamba moto
Harakati za ukombozi zikachacha usiku na mchana
Walowezi waporaji wa mashamba yetu wakachinjwa
Mahomugadi wasaliti wetu wakawawa
Mashambulizi ya jeshi la uvamizi la mkoloni
Yakajibiwa na jeshi la haki la kizalendo
Yakajibiwa yakajiwa mashambulizi ya adui yakajibiwa
Dawa ya moto ikawa ni moto
Serikali ya Mwingereza Kenya
Ikawa inakukutishwa hasara juu ya hasara
Watu wetu wakazidisha usanii katika vita vya ukombozi
Bunduki zikawa zinatengenezwa Nyandarwa na Kirinyagha
Mabomu na magurunedi yakawa yanaundwa Mathare na Kariobangi
Ndege za kivita za wadhalimu wetu
Zikawa zinaangushwa kila siku
Magereza yaliyokuwa yanafunga wananchi
Yakashambuliwa na wafungwa kufunguliwa na ndugu zao
Wagandamizaji wanyonyaji wavamizi wa taifa letu
Wakajiharia kwa woga wasiweze kulala usingizi
Maarifa yakawakimbia kichaa cha kupigwa pigo kikawapanda
Wakawa wanashika wanatesa wanafunga wanahamisha wanaua ovyo
Nduli wakazingira vijiji kwa maaskari na mitaro
Vikawa kama magereza kwa kuzidi kwa nyanyaso
Mateso yakawa makubwa mno mfanowe ya fashisti Hitler
Watoto wadogo wakiteswa na kupigwa na kuchinjwachinjwa
Mama zao wakitendewa ubaradhuli wakibakwa na kunajisiwa
Wananchi wakageuzwa watumwa kwa sulubu ya mabavu
Njaa na vitisho na hofu yakawa sehemu ya maisha vijijini
Mkoa wa Kati ukawa kama jehenamu kwa ukatili wa Wazungu
Jela kote nchini zikafurikana jinsi wazalendo walivyofungwa
Mashujaa wa nchi yetu wakishtakiwa na kunyongwa kila siku
Haki za binadamu Kenya zikikanyagwa na kuvunjwavunjwa kiholela
Dhambi walizotutendea wakoloni hatutazisahau hatutazisahau
Uhaini wa mahomugadi tutaukumbuka tutaukumbuka daima
Wakoloni wakatumia kila njia
Kujaribu kuuzima moto wa mapambano ya uhuru
Redio zao zikawa za kukashifu na kulaani mapambano yetu
Magazeti yao yakihalalisha ufashisti dhidi ya wananchi wa Kenya
Wakatumia hata dini, makanisa
Kujaribu kuuzima moto wa uhuru usozimika
Wapi! Wakaambulia patupu wakabaki kula mwande ole wao
Wakulima na wafanyikazi wa Kenya wasirudi nyuma wasisarende
Moto wa uhuru ukawa unawaka zaidi na zaidi kila siku unazidi

Milio ya bunduki za wazalendo za kudai haki isiwache kusikika
Damu ya walowezi na wasaliti ikawa inamwagika inamwagika tu
Historia ya mapambano
Ikaandikwa kwa wino wa damu ya wazalendo
Sifa za Mau Mau zikawa zinaenea kama upepo wa kaskazi
Zikaenea Mashariki na Magharibi na Kusini na Kaskazini pia
Afrika yote ikajivunia Mau Mau ikaonyesha njia ya kudai uhuru
Ikawa wakati Wacuba na Wakorea wanapigana dhidi ya ubeberu
Nasi huku Kenya tunapigana dhidi ya adui sampuli hiyo hiyo tu
Mau Mau ikawa mfano mkubwa sana
Kwa mataifa yanayonyonywa na kugandamizwa
Hatimaye wakoloni wakainua mikono wadhalimu wakasarenda
Wakoloni kwa hakika wakakubali kushindwa ikawapasa wakubali
Waliyojigamba hawawezekani wakawezekana Mau Mau wakawaweza
Bendera ya ufalme wa Wingereza Kenya ikateremshwa kwa aibu
Nayo bendera ya Mwafrika ya Mkenya tukaipandisha kwa hoyehoye
Historia ya ukoloni-mkongwe Kenya ikamalizika ikakwisha ikahiliki
Bali ile ya ubeberu ikawa haijakwisha kumbe haijamalizika ipo tu!
Ukoloni-mamboleo ukabisha hodi
Serikali ya Kenyatta-Kanu-Kadu
Ikasema karibu ukoloni-mamboleo karibu Kenya!
Ndipo ikawa hadi wa leo
Tunasema aluta kuntinuaaaaaahhh!!!!!!!!!
Mau Mau walitimiza jukumu lao
Nasi twaendelea kwa uzi ule ule
Idumu Mau Mau!
Udumu moyo wa kizalendo daima!

Mwandawiro Mghanga, Jela Kuu ya Kibos 3/5/1988

1. Utangulizi

Katika insha hii, kufikia sasa, tumejitahidi kusisitiza kuwa, kama jamii ya binadamu, demokrasi ina historia yake. Ili kufahamu maana ya demokrasi, ni muhimu kuielewa historia ya kale na ya sasa ya jamii inayohusika. Vilevile ni muhimu kufahamu harakati za kitabaka za taifa na kimataifa. Tutaendelea kufafanua maana ya demokrasi Kenya kwa mkabala huu huku tukikumbuka na kuyazingatia yote tuliyoyajadili hadi sasa.

2. Jamii za bara la Kenya kabla ya uvamizi wa ukoloni

2.1. Mfumo wa umajumui uliyokomaa

Kabla ya kuvamiwa na ukoloni, makabila ya Kenya, isipokuwa yale ya Waswahili katika ufuo wa Bahari Hindi na visiwa vyake, yalikuwa katika mfumo ambao tunaweza kuuita hapa, mfumo wa umajumui uliyokomaa. *Mfumo wa umajumui uliyokomaa ni kiwango cha juu zaidi cha mfumo wa umajumui halisi***.** Katika kiwango hiki, mfumo wa umajumui umekua ukakomaa na kufikia kilele chake ambapo sharti ukaondoke ili uupishe mfumo mwingine mpya na wa hali ya juu zaidi. Ni muhimu kutaja hapa kuwa kulikuwa na tofauti za kimaendeleo na kitamaduni za mamia ya maelfu ya miaka baina ya mfumo wa umajumui-halisi na mfumo wa umajumui-uliyokomaa.

Kwani katika mfumo wa umajumui halisi, binadamu alikuwa nyuma sana kimaendeleo. Hii ina maana kuwa alikuwa akitegemea maumbile kwa kiasi kikubwa sana na kwa kila hali. Pengo kati ya binadamu na wanyama lilikuwa kidogo sana tukilinganisha na binadamu wa leo. Kiwango chake cha kuyaelewa na kuyatumia maumbile kwa manufaa yake kilikuwa cha chini mno. Binadamu wa umajumui halisi alikuwa akitegemea usasi wa kishenzi na matunda na mizizi ya porini kwa ajili ya chakula. Alikuwa akiishi mapangoni, chini ya miti na katika maskani ya kishenzi.

Kinyume cha propanda za kuuhalalisha ukoloni, mataifa ya Kenya, Wamijikenda, Wajaluo, Waluhya, Wadawida, Wakalenjin, Wakamba, Wakisii, Wagikuyu, Wameru, n.k. hawakuwa wanaishi mapangoni ama chini ya miti huku wakitegemea. Watu wetu walikuwa wamepiga na wakiendelea kupiga hatua kubwa mbele za kitamaduni.

Walikuwa na kilimo cha mimea, mifugo na ndege. Walikuwa wanatumia vifaa vya shaba na chuma, ishara ya maendeleo makubwa ya sayansi, sanaa na ufundi. Walikuwa wakiishi kwa nyumba bora kulingana na wakati wao. Kulikuwa na dalili zote kwamba walikuwa wakiendelea kuongeza ujuzi wao wa kuzielewa sheria zinazotawala maumbile na kuzitumia kuongeza uhuru wao. Waliishi kufungamana na mila, ada na taratibu halisi za kisiasa na kiuchumi.

2.2. Mahusiano ya kijamii-kiuchumi ya mfumo wa umajumui

Bali, ijapokuwa Wakenya wengi walikuwa katika mfumo wa umajumui uliyokomaa na ambao ulikuwa maelfu ya miaka kimaendeleo mbele ya mfumo wa umajumui halisi, bado kuliendelea kukuwepo kwa mahusiano ya umajumui-halisi katika mfumo wa umajumui-uliyokomaa. Hii ni kwa sababu nyenzo za uzalishaji hubadilika haraka zaidi kuliko mahusiano ya uzalishaji.

Kwa mfano, hapakuwa na mali ya binafsi katika mfumo wa umajumui-uliyokomaa. Kwani *mali ya binafsi ni ile mali inayokua na kuongezeka kutokana na mfumo ambapo watu wachache wanamiliki njia kuu za uzalishaji mali na hivyo kuwa na uwezo wa kuwanyonya wengi wasio na umilikaji wa njia kuu za uzalishaji na ambao hawana budi kuishi kwa kuuza nguvukazi yao kwa njia moja ama nyingine.*

Njia kuu ya uzalishaji katika uchumi wa kilimo na ufugaji ilimilikiwa na jamaa na jamii yote kwa pamoja wala siyo watu binafsi. Nao uchumi ulikuwa umepangwa kutosheleza mahitaji ya jamaa na jamii kwa ujumla. Kila mtu mwenye afya na uwezo alishiriki katika kufanya kazi ya kutafuta riziki na kuzalisha mali kufungamana na taratibu za uzalishaji katika jamii iliyohusika. Na kila mtu alikula matunda ya jasho lake kwani hapakuwa na tabaka la wafanyikazi na lile la wanaofaidi kwa kufanyiwa kazi. Hii ina maana kwamba *matabaka na harakati za kitabaka hazikujulikana Kenya ya bara kabla ya kuwasili kwa ukoloni.*

2.3. **Hapakuwa na dola kabla ya ukoloni**

Katika hali hii, *dola tunayoifahamu kama mashini ya tabaka moja ya kutawala na kunyanyasa tabaka lingine, haikuwako katika makabila ya bara la Kenya kabla ya uvamizi wa ukoloni.* Dola halikuwako kwa kuwa halikuhitajika. Watu walipanga maisha yao kwa taratibu maalumu iliyowawezesha kuishi kwa amani na salama bila kutumia vyombo vya dola vya kutisha, kushurutisha na kugandamiza. Badala ya sheria kama tunavyozifahamu leo, watu wa makabila ya bara la Kenya walitumia maadili yao yaliyokuwa na msingi wake katika mfumo wa umajumui -uliyokomaa. Badala ya katiba, sheria, polisi, magereza, majeshi na serikali walitumia mila, ada, miko, imani za ushirika mkiwemo dini - kwa ufupi tamaduni - kutawala jamaa, jamii, kuhifadhi amani na utangamano na kulinda na kuendeleza amani na utangamano katika jamii.

Wazee walikuwa na nafasi muhimu sana katika jamii ya mfumo wa umajumui uliyokomaa. Wazee wanaume ndiyo waliyokuwa na madaraka ya kujadiliana na kupitisha maamuzi makuu ya jamii. Baraza la wazee (wa kiume) ndilo lililojumuika kama mahakama wakati kulipokuwa na mahitaji ya kusuluhisha mizozo fulani katika jamii, kupatanisha jamaa, kuamua kesi zozote zilizojitokeze kama za mauaji, dhuluma, ugomvi, wizi, n.k.

Hapakuwa na jeshi la kudumu bali wakati walipolazimika kupigana vita, wazee walipiga mbiu ya mgambo kuwakusanya watu kwa mikutano ili kupitisha maamuzi kuhusu vita na kuwazatiti vijana kutwaa nyuta na mishale, ngao na mikuki. Kwa sababu hii, tunaweza kusema kwamba, *ingawa makabila yote ya Kenya yalikuwa na taratibu maalumu za kuendesha maisha yao, kuhakikisha kuna amani na utangamano na kusuluhisha matatizo ya kijamii, hapakuwa na demokrasi kama taratibu maalumu inayoshirikiana na dola kunyanyasa tabaka lingine katika jamii.*

2.4. **Dalili za mfumo wa kitabaka zilikuwa zimejitokeza kabla ya ukoloni**

Pamoja na haya yote, ni muhimu kukumbuka kuwa ingawa mfumo wa umajumui –uliyokomaa - kama tunavyouita historia ya makabila ya bara la Kenya kabla ya kuvamiwa na ukoloni - ulikuwa bado na masalia mengi ya adili ya mfumo wa umajumui-halisi, vilevile wakati wote ulikuwa ukikua na kubadilika. Tayari ulianza kuonyesha dalili za mfumo wa kitabaka.

Kulianza kuibuka na kukua kundi la watu ambao walikuwa na mashamba makubwa zaidi, mifugo mingi zaidi na jamaa kubwa zaidi kuwaliko wengine. Hawa walianza kuwa na sauti zaidi katika mabaraza ya wazee kuwaliko watu wengine kwani walikuwa na uwezo wa kuzalisha ziada kubwa zaidi.

Katika jamii ya Wakikuyu, kwa mfano, kulitokea kundi la watu ambao waliitwa *wahoi*. Wahoi hawakuwa na ardhi ama kwa sababu moja ama nyingine waliishi kwa jamaa zingine na kujipatia riziki kwa kuwafanyia kazi jamaa hizo. Bila shaka wahoi hawakuwa sawa na watu wa jamaa walizokuwa wakizitumikia.

Isitoshe, ni muhimu kusisitiza kwamba katika makabila ya Kenya tunayoyazungumzia, ambayo yalikuwa katika mfumo wa umajumui-uliyokomaa, wanawake hawakuwa sawa na wanaume. *Wanaume walikuwa wakiwanyanyasa sana wanawake.* Katika jamii nyingi maamuzi yote makuu ya kimsingi yalifanywa na wanaume, yawe ni maamuzi ya nyumbani ama ya kijamii. Mkuu wa jamaa alihesabiwa kuwa mwanamume. Wanawake hawakuwa na haki ya kurithi mali moja kwa moja kutoka kwa wazazi wao. Mila, ada na miko ilitumiwa kuhalalisha mahusiano ya kuwanyanyasa wanawake.

Wazee wanaume ndio waliyokuwa na haki zaidi katika jamii. Vijana na watoto walilazimishwa na mila na ada kutii wazee wao, kwani ilisemekana kuishi kwingi ni kuona mengi. Maoni na maamuzi ya wazee wanaume ndiyo yaliyokuwa yakitawala.

Kukua kwa nyenzo za uzalishaji kulileta hali mpya ya ugamvi wa kazi. Katika jamii kulikuwa na kazi za wanawake na wanaume, wazee na vijana, watoto na watu wazima. Wanawake, kwa mfano waliwachiwa kazi nyingi zaidi za nyumbani, kupika, kuteka maji, kutafuta kuni, kulea watoto, kuosha, kusafisha vyombo na nyumba, n.k. Aidha, waliwachiwa kazi za kupalilia na kupanda mimea, kuchuna mboga shambani na porini n.k. Wanawake walifanya kazi kwa muda mrefu zaidi kuwaliko wanaume. Katika jamii nyingi wanaume walifanya kazi za kuchunga mifugo, kuwinda, nk.

Katika jamii ya mfumo wa umajumui-uliyokomaa, kulikuwa kumejitokeza kundi la watabiri, waganga na wapigaramli ambao walikuwa wanatumia ujuzi wao kupata faida kutoka kwa wateja wao. Hivi ni kusema kwamba watabiri, waganga na wapigaramli walizidi kuishi kwa kuuza ujuzi wao, kwa kutumia vipawa vyao ama elimu ya urithi, kuwanyonya watu wengine.

Aidha, viongozi wa kidini, mafundi wa kila aina kama wafua vyuma, wachongaji, wafinyanzi, n.k., kila siku waliendelea kutumia elimu na ujuzi wao kuwanyonya watu wengine ambao hawakuwa na ujuzi huo. Pengine, ndiyo kwa sababu katika makabila mengi ujuzi ama ufundi kama wa uganga na upigaji ramli, ufuaji vyuma, ufinyazi, n.k., ulihodhiwa na jamaa chache tu ambazo ziliulinda na kuufanya kuwa siri yao ya ukoo.

Kwa muhtasari, *wakati ukoloni ulipotuvamia, tulikuwa tukifanya historia. Hatukuwa tumekwama. Tulikuwa tunafanya maendeleo. Tulikuwa tunatoka kutoka kwa mfumo wa umajumui-uliyokomaa na kwenda kwa mfumo wa juu zaidi. Dalili zilionyesha wazi kuwa tulikuwa tukielekea katika mfumo wa kitabaka.* Katika jamii ya Waluhya, kwa mfano, mfumo wa ukabaila ulikuwa umechipuka kama taratibu za kifalme, Nabongo wa Wanga, zinavyodhihisha. Hii ni kusema kwamba huko kwa Waluhya demokrasi ya kikabaila ilikuwa tayari imezaliwa na ilikuwa ikikua na kuenea na ufalme wa Mumia Magharibi mwa Kenya.

Tunasisitiza: haya yote yalikuwa yakiendelea kabla ya ukoloni kuvamia nchi yetu.

3. **Mfumo wa utumwa/ukabaila katika Pwani ya Kenya**

Huko pwani ya Kenya, mfumo wa ukabaila ulikuwa umezaliwa na kuwa sehemu ya utamaduni wa Waswahili kwa karne nyingi kabla ya kuwasili kwa ukoloni wa Wingereza Kenya. Nyenzo za uzalishaji zilikuwa zimekua sana na kuzalisha utamaduni wa hali ya juu kwa kila hali. Wageni wa kwanza kufika pwani ya Kenya kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, waliikuta miji kama Lamu, Pate, Siu. Takaungu, Malindi, Mombasa, Vanga, na kadhalika ikiwa na wafalme wake na ustaarabu wake.

Kwa sasa hatutajadiliana kuhusu ustaarabu wa Waswahili wakati huu kwani tukifanya hivyo tutakuwa tumetoka kwa upeo wa insha hii. Inatosha tu kukariri kwamba *Waswahili walikuwa katika kiwango cha kwanza cha mfumo wa ukabaila***.** Kulikuwa na tabaka la makabaila na mamwinyi kwa upande mmoja na lile la wajoli, matwana na watumwa kwa upande mwingine.
Dola la hali ya juu kwa kila hali lilikuwako karne nyingi kabla ya kuja kwa ukoloni. Wafalme ndiyo waliyokuwa wakishikilia nguvu za dola kwa niaba ya tabaka la makabaila. Kutokana na haja ya kuzima harakati za kitabaka na kuvamia falme jirani ama kujihami kutoka kwa uvamizi wa wageni kama Waarabu na Wazungu, mataifa ya Waswahili pwani ya Kenya yalikuwa na vikosi vya kudumu vya majeshi ya baharini na nchi kavu. Kuna ushahidi kuwa kulikuwako na mamlaka ya serikali, sheria na mahakama, polisi na magereza katika jamii za Waswahili kwa mamia ya miaka kabla ya kuwasili kwa ukoloni.

Ni kutokana na utamaduni wa hali ya juu wa kikabaila na uimara wa dola lake, ndipo Waswahili wakaweza kuutea uhuru wao na wa Kenya yote kwa ujumla, kutoka kwa Waarabu na Wareno kwa karne kadhaa. Kama si Waswahili, utawala wa Waarabu na Wareno, ungelikuwa umepenya bara na kutawala nchi yetu mamia ya miaka kabla ya ukoloni wa Wingereza. Kama si uimara wa dola la Waswahili na utamaduni wa uzalendo uliyowawezesha kutetea uhuru na demokrasi yao, madhara ya biashara ya utumwa iliyodumu hadi karne ya kumi na tisa, yangelikuwa makubwa mno pwani na bara ya Kenya.

Tukikumbuka yale tuliyoyasema katika kufafanua maana ya demokrasi katika mfumo wa ukabaila, tutafafanua *maana ya demokrasi katika ufuo wa bahari ya Kenya na visiwa vyake kwamba demokrasi ilikuwa serikali ya makabaila iliyokuwa ikiongozwa na wafalme (masultani) kwa ajili ya makabaila na kwa lengo la kuuimarisha ukabaila.* Na hii ilikuwa mamia ya miaka kabla ya ukoloni wa Wingereza kuvamia Kenya.

4. **Demokrasi wakati wa ukoloni - mkongwe**

4.1. **Madhumuni ya ukoloni**

Wakoloni hawakuvamia nchi yetu ili kutustaarabisha. Tulikuwa na ustaarabu wetu wenyewe tangu kale na zamani. Kama tulivyosema, hapo awali, tulikuwa tunapiga hatua mbele kwa kila hali. Wazungu hawakutoka Ulaya kuja katika nchi yetu ili kutuelimisha, kutufunza dini, kutuonyesha njia za maendeleo na kutufanyia mema kama wanavyodai.

Lengo la kimsingi la ukoloni lilikuwa ni kunyonya na kupora nchi yetu. *Ukoloni ulikuwa sehemu ya ubepari wa Wingereza ambao ulifikia kiwango cha ubeberu cha kuweza kusafirisha ziada ya mtaji hadi nchi yetu.* Wakoloni walikuja kwetu kutafuta soko, malighafi na nguvukazi rahisi kwa ajili ya viwanda vyao na bidhaa zao. Wazungu walitumia visababu mbalimbali kama kueneza ukiristo bali lengo lao hasa lilikuwa ni kujitajirisha kutokana na jasho letu na rasilimali za nchi yetu.

4.2. **Ukoloni uliingia Kenya kwa nguvu za dola**

Tena ukoloni haukubisha hodi Kenya. Hatukuukaribisha ukoloni. Kinyume chake *historia ya Kenya inadhihirisha kwamba watu wa Kenya waliupinga ukoloni tangu mwanzo kabisa.* Kwani ukoloni ulituvamia. Wakoloni waliingia Kenya kwa mabavu, kwa mitutu ya bunduki. Wakoloni walijenga dola la kikoloni Kenya. *Nalo dola la kikoloni lilikuwa na madhumuni ya kuuimarisha na kuutetea mfumo wa ukoloni na maslahi ya kikoloni ya Wingereza katika nchi yetu. Dola la Wingereza Kenya lilikuwa mashini ya wakoloni ya kuwatawala, kuwanyonya na kuwanyanyasa Wakenya wote kwa ujumla.*

Magavana walikuwa wakuu wa serikali ya kikoloni Kenya na kazi yao ilikuwa ni kuhakikisha ukoloni wa Wingereza unakua, unaimarika na unaendelea kuwanyonya na kuwanyanyasa Wakenya kwa manufaa ya Wingereza. Serikali ya kikoloni Kenya, haikuchaguliwa na Wakenya, haikukubaliwa na Wakenya na wala isingeliweza kutambuliwa wala kukubaliwa na wazalendo. Ilikuwa ni serikali ambayo haikuhesabu wananchi wa Kenya kama watu. Chini ya ukoloni Wakenya walichukuliwa kama mifugo wa kutumiwa kwa ajili ya Wingereza. Chini ya ukoloni, taifa letu lilifanywa ng'ombe mkubwa wa kukamwa Wingereza.

Sheria na mahakama yalitumiwa kuwatawala Wakenya kwa mabavu. Wakenya hawakushirikishwa katika kutunga sheria ambazo zilitumiwa kuwalazimisha kuutii ukoloni, kulipa kodi, kubeba vipande, kufanya kazi ya shokoa na kunyonywa katika mashamba, nyumba na viwanda vya walowezi.

Polisi walitumiwa kuwasaka, kuwakamata, kuwatesa na kuwaua Wakenya wote waliyokataa kufuata sheria za kidhalimu za kikoloni. Na kutii sheria za kikoloni kulikuwa na maana mtu akubali kuutambua ukoloni, kubaguliwa, kutawalwa, kunyonywa na kunyanyaswa na wageni katika nchi yako mwenyewe. Na kwa vile siku zote Wakenya walikuwa wakiugomea ukoloni, kwa njia moja ama nyingine, magereza yalijengwa na wakoloni na kutumiwa kuwafunga maelfu kwa maelfu ya wazalendo waliyokuwa wakizivunja sheria dhalimu za kikoloni kila siku.

Nalo jeshi la kikoloni liliundwa na kuwekwa tayari kila mara kupigana dhidi ya umoja ama mshikamano wowote wa kupigania uhuru na ukombozi wa kitaifa. Kwa kutumia vyombo vya dola la kibepari, wakoloni waliwaua maelfu kwa maelfu ya Wakenya wasiyo na hatia. Wakenya walinyang'anywa mashamba, mifugo, mali na haki za binadamu na watu weupe katika nchi yao wenyewe.

4.3. **Wakoloni walipiga vita tamaduni za Wakenya**

Kwa kutumia itikadi ya ubaguzi wa rangi kuwanyonya na kuwagandamiza Wakenya, watu weusi tulihesabiwa kama watu wa mwisho katika nchi yetu yenyewe, tukisemwa kuwa hatukuwa watu kamili kama watu weupe. Utamaduni wetu ukapigwa vita na wakoloni kwa kutumia dola lao na dini yao. Ikawa inafundishwa ati sisi watu weusi, sisi Wafrika ati hatukuwa tumegundua kitu chochote kile kabla ya kuwasili kwa ukoloni! Ati historia yetu ilianza kwa kuja kwa watu weupe Kenya!

Kwa kutumia dola, ukoloni ulijitahidi kuvuruga maisha tuliyokuwa tukiishi kabla ya ukoloni. Wakenya tukajikuta tunapachikwa mahusiano mapya ya kibepari ya unyonyaji na udhalimu wa mtu kwa mtu ambayo hayakuwa na msingi wowote katika historia yetu na utamaduni wetu. Hata hivyo, ukoloni ulikuwa unatubandika mfumo wa kibepari pasina uchumi wa ubepari wenye mizizi yake ndani ya nchi yetu na demokrasi ya kibepari.

4.4. **Demokrasi ya ukoloni**

Kwani *wakati wa ukoloni-mkongwe, demokrasi ilikuwa ni serikali ya wakoloni iliyokuwa ikiongozwa na wawakilishi wa serikali ya kifalme ya Wingereza kwa ajili ya walowezi, wakoloni na ukoloni wa Wingereza.*
Huu ndiyo unafiki wa demokrasi ya kibepari! Wakati wananchi wa Wingereza angalawa walikuwa wakiishi chini ya demokrasi ya kibepari, Wakenya walikuwa wakiishi chini ya ufashisti. Wakenya waliporwa haki zote zinazofanya demokrasi ya kibepari. Walikuwa wakitawalwa na wageni katika nchi yao wenyewe. Walikuwa wamenyang'anywa haki ya kuchagua serikali, kuwa na vyama vya kisiasa na vya wafanyikazi, kukutana, kuongea, kusafiri pahali wanapotaka na wakati wanapopenda, kuandamana, kusoma kile wanachokitaka na kadhalika.

Demokrasi ya wakati wa ukoloni ilikuwa ya kikoloni. Sheria za kikoloni zilikuwa za kuvunja haki za binadamu za Wakenya. Ni wakoloni, walowezi, watu weupe tu ambao walikuwa wakifurahia demokrasi ya kibepari Kenya, demokrasi ambayo ilikuwa Wingereza wakati huo huo! Kwa mfano, kina Bildard Kaggia na Jomo Kenyatta walikutana na demokrasi ya kibepari mara ya kwanza waliposafiri Ulaya kwani siku zote wakiwa Kenya walikuwa chini ya imla ya ukoloni wa Wingereza. *Demokrasi ya kibepari Ulaya, ufashisti Afrika wakati huo huo: ni unafiki wa demokrasi ya kibepari!*

4.5. **Kupigania uhuru kulikuwa kupigana dhidi ya demokrasi ya kikoloni**

Kwa sababu hii, *mapambano ya uhuru na ukombozi ya Wakenya, vilevile yalikuwa mapambano dhidi ya demokrasi ya kikoloni*. Na kila marekebisho waliyoyanyakua kutoka kwa wakoloni, kama kuruhusiwa kuanza kuwa na wawakilishi katika bunge la wakoloni, kufanya mikutano na maandamano, kuunda vyama vya kisiasa, kuanzisha vyama vya wafanyikazi, kuwacha kubeba vipande, kupanda mimea ya biashara kama kahawa na chai, kudai uhuru kwa kutumia katiba ya kikoloni na kadhalika, yote haya yalikuwa hatua mbele kuelekea kwa uhuru na yalitokana na mapambano makali dhidi ya demokrasi ya kikoloni. Wazalendo wengi walisakwa, walikamatwa,

walifungwa, waliteswa, walidhalilishwa na hata kuuawa kiholela kwa kushiriki mapambano haya ya kupigania heshima na utu wa Mwafrika kwa kukataa ukoloni na demokrasi yake.

5. **Mapambano ya ukombozi kutoka kwa ukoloni**

5.1. **Mkondo wa usabili wa kudai uhuru wa kitaifa**

Msingi wa harakati za kupigania uhuru wa kitaifa ulikuwa umma wa wafanyikazi na wakulima wa Kenya. Wananchi wa Kenya waliongozwa na mikondo miwili ya kiitikadi ambayo ilitofautiana katika mbinu za kupigania uhuru na malengo ya uhuru wenyewe.

Kuna mkondo uliyokuwa umechagua kupigania uhuru kwa kutumia njia za kiamani na kikatiba peke yake. Hata katika hali ambapo wakoloni walitangaza hali ya hatari, ufashisti dhidi ya Wakenya, mkondo huu uliyoongozwa na mabepari-mchwara waliendelea kujitenga na mapambano ya kutumia silaha yaliyokuwa yakiendelea. Badala yake wakachagua kujadiliana na wakoloni pasina kuwazatiti na kuwaongoza wananchi kupigania ukombozi wao kwa vyovyote vile, hata kwa kutumia silaha.

Vyama vya Kenya African National Union (KANU) - mkondo wa kina Jomo Kenyatta - na Kenya African Democratic Union (KADU) viliongozwa na watu wa mkondo huu ingawa KANU wakati huo ilikuwa inawakilisha sauti ya wananchi wengi wa Kenya, hata waliyokuwa wamechukua silaha, ya kudai uhuru wa kitaifa mara moja na bila kuchelewa. Hii ni kwa sababu uongozi wa KANU ulikuwa na viongozi wachache wazalendo, wenye sasa kali, kama kina Jaramogi Oginga Odinga, Bildada Kaggia, Achieng' Oneko, Fred Kubbai, tawi la KANU la Nairobi na Taita, pamoja na wafuasi wengi kutoka kwa tabaka la wafanyikazi na umma wa Kenya kwa ujumla.

Lakini KADU, chama kilichokuwa cha kina Ronald Ngala na Daniel Toroitich arap Moi, kilifuata siasa za kuwa mtoto mzuri wa wakoloni na walowezi wakati wote. Si ajabu, kwa hivyo, kwamba KADU ilikuwa ikipigania kuahirishwa kwa uhuru wa Kenya hadi mwaka wa 1988 na kupinga umoja wa kitaifa!

Bali, vilevile, inajulikana kwamba baada ya kukwamuliwa kwa ukoloni-mkongwe, haikuchukuwa muda kabla KANU na KADU hawajaungana kupambana dhidi ya wale wote ndani ya vyama hivyo na nchini waliyoendelea kudai demokrasi ya wananchi wengi na uhuru kamili. Maana waliyochukua hatama zaserikali baada ya kuondolewa kwa ukoloni mkongwe – wakiongozwa na rais wa kwanza wa Kenya – Jomo Kenyatta, waliamua kurithi demokrasi ya kikoloni ya kuwagandamiza makabwela.

5.2. **Mkondo wa kimapinduzi wa kudai uhuru wa kitaifa**

Mkondo wa Jeshi la Uhuru na Mashamba – maarufu kama Mau Mau - ulichagua kupigania uhuru wa Kenya kwa kutumia silaha. Baada ya kuona kuwa wakoloni walikuwa wanayapuuza madai ya uhuru kupitia kwa njia za kiamani, na baada ya kugundua ukweli kuwa katiba na dola lote la kikoloni lilikuwa limejengwa na kuimarishwa kwa madhumuni ya kufanya Kenya kuwa koloni la Wingereza milele, wafanyikazi na wakulima makabwela wa Kenya wakaona hawana budi ila kuchukua silaha na kutangaza vita dhidi ya dola la kikoloni.

Mau Mau walielewa vizuri kwamba kupigania uhuru kutoka kwa ukoloni ni kupigana dhidi ya dola la kikoloni. Mau Mau waliongozwa na imani kwamba kadiri mdhalimu anaendelea kudhibiti na kuhodhi uwezo wa kivita dhidi ya wadhulumiwa, ataendelea kuwadhulumu kwa kiburi na

wala hatakubali hata kujadiliana nao kwa misingi ya haki na usawa. Ndipo kukawa hakuna budi ila kuunda Jeshi la Uhuru na Mashamba.

Wakati mikondo ya wasabili ya KANU na KADU walikuwa wakidai uhuru kwa njia za marekebisho, Mau Mau walichagua njia ya kimapinduzi. Jina halisi la Mau Mau ni Jeshi la Uhuru na Mashamba nalo linaonyesha kuwa Mau Mau walikuwa wanapigania demokrasi ambayo itawawezesha wananchi wote kuwa na njia za kujipatia kumiliki maliasili, mkiwemo ardhi. Mau Mau walikuwa na hakika kabisa kwamba pasina wananchi wote kurudishiwa mashamba waliyokuwa wamenyang'anywa na wakoloni; pasina kuwa na mipango ya kiuchumi na kisiasa ya kuhakikisha kuwa kila Mkenya ana nafasi na njia ya kumwezesha kuishi maisha ya kiutu; pasina kutekelezwa kwa haki za binadamu mkiwemo haki za kiuchumi na kijamii; Kenya haiwezi kusemekana iko huru. Haya ndiyo pia yalikuwa matarajio ya wananchi wengi wa Kenya ambao waliunga mkono Mau Mau na KANU (ya wakati huo) na kushiriki katika harakati za kupigania uhuru na ukombozi wa taifa letu.

5.3. **Njama za ukoloni-mamboleo na vibaraka wake**

Lakini, kama walivyokuja kufahamu baada ya kukwamuliwa kwa ukoloni-mkongwe, *uhuru uliyokuwa ukipiganiwa na viongozi wengi wa KANU na KADU haukuwa sawa na ule uliyokuwa ukipiganiwa na Jeshi la Uhuru na Mashamba (Mau Mau) na wananchi wengi wa Kenya.*

Mapambano ya silaha ya Jeshi la Uhuru na Mashamba, ndiyo yaliyowalazimisha wakoloni kukubali kujadiliana na Wakenya kuhusu uhuru. Lakini wale waliyoshiriki katika majadiliano ya uhuru wa Kenya nchini Kenya na huko Wingereza siyo wale waliyowalazimisha wakoloni kukubali majadiliano. Si kina Dedan Kimaathi na Mau Mau. Wale waliyopigania uhuru kwa njia za marekebisho na ubarakala, kina Jomo Kenyatta na kina Tom Mboya na KANU yao, na wale ambao walikuwa vibaraka vya walowezi, waliyokuwa wakipigania kuahirishwa kwa uhuru na siasa za majimbo za kuligawanya taifa letu kikabila, kina Ronald Ngala na kina Daniel Toroitich Arap Moi na KADU, ndiyo waliyojadiliana na wakoloni na kukubaliana nao kuhusu"uhuru" wa nchi yetu! Kwa njia hii harakati za ukombozi wa Kenya za kuondoa demokrasi ya kikoloni na badala yake kuleta demokrasi ya uhuru wa kijamii na kitaifa – harakati za ukombozi zikaparaganywa na kutekwa nyara na vibaraka wa wakoloni wakiongozwa na Jomo Kenyatta.

6. **Ukolonimamboleo**

6.1. **Njia za marekebisho hazikung’oa mizizi ya ukoloni**

Kutokana na hayo yote tuliyoyasema kuhusu mapambano ya uhuru, tunaona kwamba ukolonimkongwe ulitoka kwa mlango wa mbele na kurudi hapo hapo sawia kama ukolonimamboleo kwa kupitia kwa mlango wa nyuma.

Tulisema kuwa KANU, KADU na mikondo mingine yote ya kudai uhuru, walichagua barabara ya marekebisho. Ni Mau Mau tu waliyochagua njia ya kimapinduzi ya kupambania uhuru, kwani Mau Mau walikataa kulitambua dola la kikoloni na wakakata shauri kupambana kuling'oa.

Bali kutokana na hali halisi ya kihistoria ambayo hawangeweza kuiepuka, (tutaizungumzia kwa kirefu tutakapojadiliana kuhusu Mau Mau) ukosefu wa nadharia ya kimapinduzi ulisababisha vitendo vya kimapinduzi vya Mau Mau kukosa kuleta mapinduzi katika nchi yetu. Maana *bila nadharia ya kimapinduzi hapawezi kuwa na harakati za kimapinduzi zinazoweza kuwaongoza wanaonyanyaswa kujikomboa kabisa.*

Njia za marekebisho hazikuuvunjilia mbali mfumo wa ukoloni na kuwakomboa wananchi wa Kenya na taifa lao. Njia za kudai uhuru kufungamana na demokrasi ya kibepari na kikoloni zilifaulu tu kubadilisha sura ya ukoloni na kubakisha msingi wa ukoloni ukiwa madhubuti.

6.2. **Dola la Kenya la leo limerithiwa kutoka kwa ukoloni**

Serikali ya Jomo Kenyatta na KANU - KADU iliyochukuwa madaraka ya kutawala kutoka kwa wakoloni, ilirithi mfumo wa kikoloni-kibepari na dola lote la kikoloni.

Katiba ya kitaifa ya Kenya, haikuwa katiba ya Wakenya iliyoundwa na Wakenya kwa ajili ya Wakenya. Ilikuwa ni katiba iliyopachikwa watu wa Kenya na wakoloni na vibaraka wake ili kujenga na kuimarisha mahusiano ya kibepari-kikoloni. Karibu sheria zote za Kenya ni zilezile zilizotungwa na wakoloni ili kuwatawala, kuwanyonya na kuwagandamiza Wakenya. Muundo, sura na malengo ya mahakama ya kikoloni ya kulinda mali ya binafsi, kutetea maslahi ya wachache dhidi ya wengi, kuutetea mfumo wa udikteta, haukubadilika na wala haujabadilika hadi wa leo.

Mfumo wa polisi uliyokusudiwa kuutetea ukoloni, kupinga haki za wengi, kutekeleza sheria za kikoloni, kuwatisha, kuwahofisha na kuwagandamiza wananchi nao ulirithiwa pasina mabadiliko yoyote ya kimsingi.

Magereza yaliyokuwa na lengo la kuwafunga, kuwatesa na kuwatenga wazalendo na mashujaa wa uhuru, kuwazuia wote waliyokuwa wakitisha usalama wa mali ya binafsi, yalirithiwa hivyo hivyo baada ya 'uhuru'. Tofauti ni kwamba wafungwa wengi wanasema kwamba hali ya wafungwa magerezani ni mbaya zaidi hivi leo hata kuliko wakati wa ukoloni-mkongwe!

Jeshi lililokuwa likipambana dhidi ya Mau Mau na harakati za wananchi wa Kenya, likarithiwa na "Kenya huru" na lile la Mau Mau likavunjwa. Ndiyo kwa maana jeshi la Kenya limetumiwa kuvunja haki za binadamu, kutetea tawala za imla na hata kufanya uhalifu dhidi ya binadamu, hasa Kaskazini Mashariki mwa nchi yetu.

Wale Wakenya waliyokuwa wakiutumikia ukoloni kwa kila hali, machifu, watoto wa machifu, viongozi wa makanisa mbalimbali na mahomugadi, wakachukuwa madaraka tena baada ya kukwamuliwa kwa ukoloni mkongwe. Wasaliti, waliyokuwa wakiuza nchi yetu kwa pesa nane, waliyokuwa wakiwatesa na kuwauwa Wakenya waliyokuwa wakiupinga ukoloni, waliyofanya madhambi makubwa mno ya kuvunja haki za binadamu katika ari na ghera ya kuutumikia ukoloni, wakapandishwa vyeo vya kuongoza serikali ya usaliti ya Kenyatta-Kanu-Kadu. Mfumo wa utawala wa umma wa kutekeleza amri na sheria za kidhalimu nao vilevile ukarithiwa. Mahomugadi na vibaraka wa wakoloni wakachukua nyadhifa za ma-Katibu Wakuu, ma-PC, ma-DC, ma-DO, ma-Chifu na wakuu wa serikali kwa ujumla.

Wakati huo huo, utawala wa Kenyatta-Kanu-Kadu, mara tu baada ya kuchukuwa nafasi ya wakoloni ya kuwatawala Wakenya, ukatangaza vita dhidi ya Mau Mau, dhidi ya mkondo wa kimaendeleo wa KANU wa kina Jaramogi Odinga, Bildad Kaggia na wazalendo wote waliyokuwa kwa KANU, na dhidi ya wakulima na wafanyikazi na wananchi wengi kwa ujumla ambao waliendelea kushikilia mwito: *Uhuru na Mashamba*!

Badala yake, serikali ya Kenyatta ikaunda mwito mpya:*Uhuru na Kazi*!- siyo kazi ya kuwakomboa wananchi wengi kutoka kwa maisha ya dhiki na umaskini, bali kazi ya kuwatajirisha wanyonyaji wa kienyeji na wale wa nchi za nje. Kazi ya kuwatumikia Wazungu

Weusi au vibaraka wa mabeberu kwa mashamba makubwa ambayo waliyaarithi kutoka kwa walowezi. Kazi ya vibarua mathalani shokoa katika viwanda na makampuni ya wakoloni mamboleo. Mwito wa *uhuru na kazi* wa Kenyatta ulikuwa na maana ya Wakenya wengi kukubali mfumo wa unyonyaji wa mtu kwa mtu. Kwani ikiwa *wakati wa ukoloni-mkongwe Wingereza peke yake ndiyo iliyokuwa imejinyakulia "haki" ya kunyonya nchi yetu, ukoloni-mamboleo una maana kuwa mabeberu wa USA, Ulaya Magharibi, Japan na duniani kote hivi sasa "wamejishindia haki" ya kunyonya na kufukarisha nchi yetu.*

7. **Nguzo ya ukoloni - mamboleo**

Ukoloni-mamboleo umefaulu kumea mizizi katika nchi yetu kwa kuwa nguvu za dola ziko mikononi mwa vibaraka wake, tangu wakati wa Kenyatta hadi.. Kwa kuwa utawala wa vibaraka wa mabeberu ni utawala wa kupinga maendeleo, uhuru na ukombozi wa kitaifa, unachukiwa sana na umma. Kwa sababu hii unatawala kwa mitutu ya bunduki.

Vibaraka wa mabeberu, tabaka linalodhibiti nguvu za dola na ambalo ni tabaka la wanyapara wa mitaji ya mabeberu nchini, tabaka la wabakuzi wa mashamba na maploti, tabaka la matajiri na mamilionea wa kienyeji, wamekuwa wakitawala kwa mabavu, tangu wakati wa Kenyatta hadi leo wakati wa Moi.

Demokrasi iliyoko Kenya leo ni serikali ya wanyonyaji, tabaka la vibaraka wa mabeberu, inayoongozwa Moi na Kanu na genge lake la mafia kwa ajili ya ubeberu na vibaraka wao, wanyonyaji na wasaliti wa nchi yetu. Ni demokrasi ya tabaka la watu wachache ya kulinda mfumo wa kibepari-kikoloni ambao unawanyonya na kuwanyanyasa wengi wetu na kupinga uhuru na ukombozi kitaifa.

8. **Hali halisi chini ya ukoloni-mamboleo**

Chini ya utawala wa vibaraka wa mabeberu, Wakenya wanalazimika kuishi na kutawalwa kama vile wananchi wengi wa Ulaya walivyokuwa wakiishi na kutawalwa kabla ya mapinduzi ya kibepari mnamo karne ya kumi na tisa. Haki za binadamu zinazotambuliwa na kufafanuliwa na demokrasi ya kibepari, nchini Kenya zinapuzwa na kukanyagwa kiholela.

Udikteta umeshakua na kushamiri na kuwa sehemu ya utamaduni wa nchi yetu. Nazo serikali za kibepari zinahubiri haki za binadamu huku zikiunga mkono utawala wa kiimla kwa hali na mali kadiri ambapo unatumika kulinda masilahi yao ya kibeberu.

Udikteta uliyowekwa msingi na utawala wa Jomo Kenyatta umefikia hatua ya kuwa kama ufashisti katika utawala wa Moi. Kwani utawala wa Moi hauheshimu hata katiba ama sheria ambazo ni za imla. Moi anatumia serikali, polisi na majeshi kuwakamata, kuwatesa, kuwafunga, kuwaua na kuwapora mali zao wananchi kila siku. Moi anatawala Kenya kama milki yake na mali yake ya binafsi.

Katika juhudi za kupinga demokrasi na kujaribu kutekeleza siasa za majimbo za Kadu ambazo zinakusudiwa kuvunja umoja na mshikamano wa kitaifa, utawala wa Moi unaendesha vita vya kikabila ambavyo vinaangamiza wananchi, mali zao na taifa letu. Udikiteta uliyokuwa katika mfumo wa chama kimoja, hivi sasa unakua ufashisti katika 'mfumo wa vyama vingi'! Wakenya wanajifundisha, kwa uchungu, kuwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa peke yake, hautoshi kuuondoa udikteta na kuleta anangalawa demokrasi ya kibepari! Kumbe utawala wa kiimla unaweza kuendelea hata ndani ya 'mfumo wa vyama vingi!'

Kwa mfano, Wakenya wako huru zaidi kuongea kuliko hapo awali. Maneno ambayo yalikuwa yakiwafunga wananchi kwa miaka mingi chini ya sheria ya uchochezi, sasa yanaongewa hadharani na yanaandikwa na magazeti ya kila siku. Ingawa bado udikteta unajitahidi usiku na mchana kuuimarisha utamaduni wa hofu na kimya, wananchi wanazungumza na kukosoa serikali kuliko hapo kabla ya katiba kugeuzwa na kuifanya Kenya kuwa ya mfumo wa vyama vingi tena.

Lakini wakati huo huo ufisadi wa wakuu wa serikali umezidi mara nyingi zadi kuliko awali. Mali ya umma inapondwa na kuibiwa wazi na hadharani. Imekuwa dhahiri kwa kila mwananchi kwamba tunatawalwa na genge la mafia. Unyama wa polisi umezidi mara nyingi, na utawala wa Moi unawauwa wananchi mara nyingi kuliko kabla ya huo mfumo wa vyama vingi. Mitaa ya mabanda mijini inachipuka na kukua kama vyoga. Chuki za kikabila zimezidi. Uchumi nao umeharibika hadi Kenya sasa tunategemea misaada ya chakula kutoka nchi za nje. Nayo miji yetu haipitiki wala haikaliki kwa kuzidi kwa uhalifu.

Isitoshe,"mfumo wa vyama vingi" unaotawalwa na Moi na Kanu na unakataa kuandikisha vyama vingine vya vya kisiasa, kama Chama cha Kiislamu na Safina. Nalo bunge la "mfumo wa vyama vingi" halina manufaa yoyote ya kimsingi kwa matumaini ya Wakenya wengi ya kidemokrasi. Chambilecho dikteta Moi, ‘bunge linaweza kupayuka jinsi linavyotaka, bali halitaweza kubadilisha sera yoyote ile ya serikali yangu. Kelele za chura hazimzuii ng’ombe kunywa maji.’

Kwa muhtasari, tunaendelea kuishi katika udikteta ambao umekua kama ufashisti chini ya mfumo wa vyama vingi! Katiba ya "kitaifa" ya leo, inampa raisi nguvu nyingi mno hivi kwamba Moi ni kama mfalme, mfalme ambaye anatawala nchi yetu kama milki yake binafsi na kwa ukatili na kiburi kisicho na kifani Afrika!

7. Je, tupambanie demokrasi gani na vipi?

7.1. **Mageuzi yanaletwa na mapambano**

Kila hatua ambayo tumepiga mbele kuelekea kwa demokrasi na utekelezaji wa haki za binadamu imetokana na mapambano makali ya wananchi wa Kenya ambao wananyonywa na kunyanyaswa yakiongozwa na wazalendo.

Kuondolewa kwa kifungo 2A kutoka kwa katiba ya kitaifa na kuilazamisha serikali ya Moi-Kanu kukubali kukuwepo kwa mfumo wa vyama vingi kikatiba kumeletwa na juhudi za wananchi wengi wanaodai uhuru na ukombozi.

Wakenya wengi wamekamatwa, wamefungwa, wamewekwa kizuizini, wamefutwa kazi na kuharibiwa mali zao, wamelazimishwa kuwa wakimbizi, wameuawa katika harakati za kupambana dhidi ya udikteta uliyokuwa kwa sura ya mfumo wa chama kimoja. Ingawa kuondolewa kwa kifungo cha 2A kutoka kwa katiba ya kitaifa ni hatua mbele, hata hivyo, "huo mfumo wa vyama vingi" haujaleta demokrasi, hata angalawa hiyo ya kibepari.

7.2. **Mapambano ya kidemokrasi yametekwa nyara**

Mapambano ya kidemokrasi ya wananchi wengi wa Kenya wanaonyonywa na kunyanyaswa yametekwa nyara na kukwamishwa na watu kutoka tabaka la mabepari wa kienyeji na mabepari-mchwara.

Kwa muda mrefu, tabaka la matajiri, mamilionea, wabakuzi wa mashamba na maploti, vibaraka wa mabeberu, mawakili na wasomi wa siasa za mlengo wa kulia, na kadhalika, wamekuwa wakishirikiana na Moi-Kanu na wakoloni-mamboleo kuwanyonya, kuwanyanyasa na kuwatawala wananchi wengi kwa mitutu ya bunduki. Wakati wafanyikazi, maskwata, wakulima makabwela, wanafunzi, walimu na wasomi wa kizalendo wamekuwa wakikamatwa, kuteswa, kufungwa, kugandamizwa na kuuawa na polisi, kwa kudai mageuzi ya kidemokrasi, wenye kutoka kwa tabaka la wanaotawala na wenye ukiritimba wa utajiri wa kitaifa wamekuwa wakinyamaza, wakijitia hamnazo huku wakiupamba udikteta kwa sifa za kila mbari.

Lakini raisi Moi akageuka na kuwa mfalme ambaye aliamuru kuabudiwa, sio tu na wananchi wa kawaida, bali pia na mamilionea, wanyonyaji wenzake. Ulafi wa mali wa Moi na genge lake la mafia ukaanza kuingilia hata mali za wanyonyaji na wasaliti wenzake. Mabepari wa kienyeji, hasa ambao si wa kabila la Kikalenjin, wakapigwa vita na genge la mafia la Moi na Biwott. Watu waliyokuwa wamechuma wakati wa udikteta wa Kenyatta wakawa wanapigwa vita vya kisiasa na kiuchumi na udikteta wa Moi! Na walipokataa kumtambua Moi kama mfalme, kama mwenye haki juu ya mali zao na haki zao za kunyonya na kusaliti nchi, wakawa wanafukuzwa kutoka kwa chama cha Kanu, wanafutwa kazi, wanafilisiwa kiuchumi na kisiasa. Hatimaye mamilionea hawa wakaanza hata kufungwa na kuwekwa vizuizini!

Ndipo ikatokea kwamba watu waliyokuwa wakuu wa Kanu, maafisaa wa serikali na mawaziri waliyokuwa wanautilia kuni moto wa udikteta wa Moi jana tu wakaamka na kugeuka digrii mia moja themanini na kuwa wapinzani wakali wa Moi na Kanu! Mabepari wa kienyeji na mabepari-mchwara wa kila aina wakadandia behewa la kudai mfumo wa vyama vingi asteaste!

Na wazalendo na wananchi wengi walipoulazimisha udikteta wa Moi kukubali kukuwepo kwa mfumo wa vyama vingi, viongozi wa Kanu na serikali, wafuasi wakuu wa nyayo, wapinga mageuzi, wanyonyaji na wasaliti wakawa sasa ndiyo wazalendo, wapenda demokrasi, maadui na majudasi wa Moi na Kanu, wapinzani wa ufisadi na udikteta!

Na hapa *vibarakala wa kutoka tabaka la wanyonyaji wakayateka nyara mapambano ya kidemokrasi ya umma wa Kenya, na wakaunda vyama vya kisiasa, FORD-Kenya, FORD-Asili, Democratic Party, na kadhalika ati kuwaongoza Wakenya kupigania demokrasi!* Hata mabeberu, mabalozi wa nchi za Magharibi wakiongozwa na balozi wa USA wakaruka na kuwa upande, wa wananchi wa Kenya waliyokuwa wakidai mfumo wa vyama vingi. Kina Smith Hempston wakawa wadhamini na washauri wakuu wa vyama vya upinzani kuhusu mbinu na hila za kupambania demokrasi Kenya!

3. **'Vyama vya upinzani' viliingiza wananchi kwa mtego wa udikteta!**

Mara tu baada ya Moi kulazimishwa na shinikizo za mapambano ya wananchi kukubali kuondoa kifungo cha 2A kutoka kwa katiba ya kitaifa, wazalendo wa Kenya walitoa mwito kwa Wakenya wasikubali kusajili vyama vya kisiasa na kushiriki katika uchaguzi kabla masharti kadhaa hayajatimizwa mkiwemo: kukuwepo kwa katiba mpya ya kitaifa, kujuzulu kwa serikali ya Moi, kuvunjwa kwa bunge na kuundwa kwa serikali ya mpito.
Moi alitangaza hadharani kwamba bado alikuwa akipinga mfumo wa vyama vingi na kwamba alilazimishwa kubadilisha katiba na kukubali mfumo wa vyama vingi kutokana na shinikizo za nchi za Kimagharibi na "wananchi wasiyotosheka".

Isitoshe, Moi na Kanu walitangaza kadamnasi ya Wakenya wote na dunia nzima kwamba watajitahidi kwa kila njia kuhakikisha kwamba wataendelea kushikilia madaraka ya uongozi kwa

vyovyote vile hata ndani ya mfumo wa vyama vingi. Kwa sababu hizi, Wakenya tungewezaje kumruhusu Moi na Kanu waliyokuwa madarakani kwa njia za imla na waliyokuwa wakishikilia kuudumisha udikteta wao hata chini ya mfumo wa vyama vingi, kuandikisha vyama vya kisiasa, kufanya utaratibu wa uchaguzi na kuusimamia uchaguzi huo huo wakiwa wagombezi!? Je, mbele ya chui kondoo ana haki na demokrasi?

4. **Mwito wa Kongamano Kuu ya Kitaifa**

Pili, msimamo wa wazalendo wa Kenya ulikuwa ni kufanyika kwa Kongamano Kuu ya Kitaifa ambayo pamoja na mambo mengine ingelijadiliana kuhusu Kenya tuitakayo wananchi wengi.

Kongamano Kuu ya Kitaifa ingeundwa na vyama vya kisiasa, na makundi mbalimbali kama ya wafanyikazi, wakulima, wanawake, wanafunzi, vijana, walimu, mawakili, wasomi na wataalamu, vijana, wawakilishi wa dini, na kadhalika. Kongamano Kuu la Kitaifa lingefanya kazi ya kufafanua maana ya mfumo wa vyama vingi katika hali halisi ya Kenya ya sasa na kuweka taratibu halisi za kujenga mazingira ya kufanyika kwa uchaguzi huru na kuondolewa kwa utawala wa kiimla katika historia ya Kenya.

Tatu, pamoja na shughuli ziingine, ilipendekezwa kwamba Kongamano Kuu ya Kitaifa iweke taratibu za kuivunjilia mbali katiba ya kitaifa ya Kenya ya Kenya ya sasa iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni, na kuandikwa katiba mpya ya kitaifa itakayolinda utawala wa demokrasi ya mfumo wa vyama vingi na itakayofafanua na kulinda haki za binadamu. Kwani katiba ya Kenya sasa ni katiba ya kuulinda udikteta, unyonyaji wa mtu kwa mtu, na uvunjaji wa haki za binadamu.

Lakini upinzani uliyoongozwa na tabaka la wanyonyaji wenyewe, vibaraka wa mabeberu na vibarakala: mawakili, wasomi wa kibwanyenye, wasabili na mabepari-mchwara wa kila aina, viongozi wa dini, wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali - wote wenye siasa za mlengo wa kulia - ulikataa kukubaliana na mapendekezo ya wazalendo. Wakaandikisha vyama vyao kufungamana na taratibu zilizowekwa na Moi. Wakashiriki katika uchaguzi uliyosimamiwa na serikali ya Moi-Kanu. Hata ilipokuwa wazi kuwa Moi-Kanu wanatumia nguvu za dola, rasilimali za kitaifa, mbinu za kigaidi kupambana dhidi ya wapinzani na kuhakikisha watashinda kwa vyovyote vile, 'vyama vya upinzani' vilivyosajiliwa viliendelea kushiriki katika uchaguzi huo tu! Tena bila haya wakashiriki kwa uchaguzi wakati serikali ilikataa kuvisajili vyama vingine.

Kura zikapigwa katika mazingira ambapo vyama vya upinzani havikuweza kutekeleza haki ya kufanya kampeni huru, ambapo Kanu ilikuwa ikiendesha vita vya kikabila hasa huko mikoa ya Rift valley, Nyanza, Magharibi na Kaskazini Mashariki. Pamoja na hayo yote, ’vyama vya upinzani’ vikaendelea kushiriki katika uchaguzi huo tu!

Kwa tamaa ya uongozi na ulafi wa mali bila kuongozwa na maslahi ya wananchi ya kutaka kuuangusha mfumo wa kiimla na kuleta demokrasi Kenya, 'vyama vya upinzani' vikakataa kufanya umoja dhidi ya utawala wa kishenzi na wa kupinga maendeleo zaidi wa Moi-Kanu. Badala yake wakashiriki katika uchaguzi huku kukiwa na zahama baina ya viongozi ndani ya kila chama na baina ya hivyo ‘vyama vya upinzani’! Moi-Kanu wakafurahi hata zaidi kwani vita vya panzi ni furaha ya kunguru.

Na kura zilipopigwa, kama ilivyotabiriwa, Moi-Kanu wakashinda kwa kutumia udanganyifu na nguvu za dola kama vile ‘vyama vya upinzani’ vyenyewe vilivyothibitisha. Kwa kweli uchaguzi ulikuwa umeibwa kitambo hata kabla kura hazijapigwa. Lakini pamoja na haya yote, 'vyama vya upinzani' hatimaye vikakubali kuutambua,"ushindi" wa Moi-Kanu na vikakubali kushiriki katika

bunge linaloongozwa na chama cha kupinga demokrasi na haki za binadamu - chama cha Kanu.

5. **'Vyama vya upinzani' vinayumbishwayumbishwa na mabeberu!**

Nazo nchi za kibepari ambazo zilikuwa zinajifanya (na zinaendelea kujifanya) kuwa marafiki wa mapambano ya demokrasi na uchaguzi huru na wa haki Kenya, zilivishauri 'vyama vya upinzani' kukubali kuitambua serikali ya Moi-Kanu ambayo hata wao wenyewe walikubali kinagaubaga kuwa iliendelea kujidumisha madarakani kwa kutumia nguvu za dola na udanganyifu katika uchaguzi.

Hivi sasa, mataifa ya kibepari yanaendea kuunga mkono serikali ya Moi-Kanu kwa pesa, diplomasi na propaganda kwamba ni serikali ya kidemokrasi iliyochaguliwa katika mfumo wa vyama vingi wakati ambapo Moi-Kanu wamegeuza nchi yetu kuwa mito ya damu kwa mauaji ya raia wasiyo na hatia ambayo yanaendeshwa na serikali ya Moi kwa jina la vita vya kikabila! Dola za kibepari zinaeneza uvumi ati Moi-Kanu wanendelea kudumu madarakani ati kwa kuwa hakuna upinzani thabiti na ati kwa kuwa ‘vyama vya upinzani’ vimeshindwa kuungana dhidi ya Moi. Hawatilii manani ukweli kwamba Moi-Kanu wanaendelea kudumu madarakani kwa kuwa hadi sasa hatujajishindia demokrasi, hatuna katiba mpya, bado hapajakuwa na mazingira ya kufanyika uchaguzi huru na halali. Isitoshe, shabaha ya harakati za kidemokrasi za umma wa Kenya ni siyo tu kuuondoa udikteta kwa sura ya Moi-Kanu, bali ni kung’oa mizizi yote ya mfumo wa udikteta.

6. **Uongozi wa wanyonyaji hauwezi kutufikisha kwa demokrasi ya umma**

Haya yote yanadhihirisha kwamba upinzani unaoongozwa na vibaraka wa mabeberu, wanyonyaji, wabakuzi wa mashamba na maploti, mabepari wa kienyeji, mabepari-mchwara, wanafiki na vibarakala, hauwezi kuwaongoza wananchi wa Kenya kuuangusha udikteta na kujenga demokrasi ya umma. Maslahi yao ya kitabaka, uhusiano wao na mabeberu na ubarakala wao hauwezi kuwaruhusu.

Kwa mfano, kutumia njia zingine za kupambania demokrasi kama mapambano ya umma: migomo ya wafanyikazi, wanafunzi na wakulima, maandamano ya wananchi yenye lengo la kutumia njia za kidemokrasi kuhakikisha kuwa serikali ya imla ya Moi-Kanu inashindwa kabisa kutawala, haziwezi kukubaliwa na viongozi wa ‘vyama vya upinzani’ vilivyojiandikisha hadi sasa kwani ‘ghasia za kisiasa’ zitahatarisha mamilioni wanayoyachuma katika viwanda, biashara na mitaji mingine wanayoimiliki kwa niaba ya au pamoja na mabwana zao mabeberu.

Aidha, mamilionea wanaoongoza ‘vyama vya upinzani nchini’ hawawezi kukubali kushirikiana na watu ambao wana mapendekezo ambayo yanaweza kuhatarisha uchumi wa kibepari-kikolonimamboleo. Kwani demokrasi yao haina shabaha ya kuukwamua mfumo wa ubepari na ukoloni-mamboleo bali kuuhifadhi.

Ukisoma mipango ya hivyo ‘vyama vya upinzani’, kwa mfano, utaona kuwa ni mipango kuendeleza maslahi ya kibepari na kibeberu kufungamana na masharti ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia. Ni mipango ya kufurahisha tabaka la wanyonyaji wa ndani na wa kigeni. Ni mipango ya kupambana dhidi ya mali ya umma na kuhalalisha na kutetea mali ya binafsi. Ni mipango ambayo, kwa mfano, haina mapendekezo halisi ya kutatua tatizo la mashamba, tatizo la nyumba mijini, kuondoa umaskini na kujenga uchumi utakaohakikisha kuwa kila mwananchi anaishi maisha ya kiutu. Mipango ya ‘vyama vya upinzani’ haina tofauti za

kimsingi ile ya Kanu: yote inatetea mfumo wa ubepari na ukolonimamboleo huku ikiwapaka mafuta nyuma ya chupa wananchi wengi wa Kenya wanaonyonywa na kugandamizwa.

Si ajabu basi kwamba viongozi wa ngazi za juu wa Forum for Restoration of Democracy (FORD - Kenya) wamejitokeza wazi kuwatetea waporaji wakuu wa fedha za umma, kina Patni na wakuu wa serikali ya Moi - Kanu.

Uchumi wa kibepari unawanufaisha watu wachache na kuwanyanyasa wengi. Ubepari wa Kenya ni wa ukolonimamboleo unaotunyonya na kutufukarisha kama taifa huku ukiwarushia makombo vibaraka wa mabeberu kutoka kwa tabaka la matajiri. Hivyo, vyama vinavyopigania demokrasi kwa mipango ya kibepari haviwezi kuwa vinapambana kuboresha maisha ya umma wa Kenya kwa kila hali. Ndiposa wazalendo wanasema,"Umoi bila Moi ni mbaya kama Umoi na Moi".

7. **Matumaini ya Wakenya wengi ni Kenya mpya**

Je, hii ni kusema kwamba watu wa Kenya hatuna matumaini yoyote ya kuuangusha udikteta na kujenga demokrasi katika nchi yetu? Hatuna matarajio ya kujikomboa kutoka kwa ubeberu na unyonyaji wa mtu kwa mtu? Hatuwezi kujenga mfumo utakaotuwezesha kutatua matatizo tilatila ya kijamii kama ufisadi, ukabila, uhalifu, ajali za barabara, umaskini, utamaduni wa kuoneana na kunyang'anyana, na kadhalika?

Mapambano ya wananchi wa Kenya ambayo hayajasita hata siku moja yanatangaza wazi na bayana kuwa Wakenya wanataka, wanatumaini na wanatarajia kuona mwisho wa udikteta na ubeberu na mwanzo wa demokrasi na mfumo mpya wa kujenga maisha bora na ya kiutu kwa kila mwananchi.

Kinachohitajika ni uongozi bora na mpya wa kizalendo unaoweka maslahi ya kitaifa na ya umma mbele ya maslahi ya ubinafsi na ulafi wa mali. Kinachohitajika ni itikadi ya kimapinduzi itakayoelekeza mapambano ya wananchi wengi wanaonyanyaswa kupambania demokrasi ya hali ya juu zaidi kuliko ile ya kibepari. Maana bila nadharia ya kimapinduzi hapawezi kuwa na harakati za kimapinduzi, chambilecho waanzilish wa ukomunisti Karl Marx na Fredrick Engels. Kinachohitajika ni chama cha kimapinduzi kinachoongozwa na itikadi ya kimapinduzi na chenye misingi yake katika tabaka linalonyonywa na kugandamizwa zaidi. Kinachohitajika ni wazalendo na wanamapinduzi wa Kenya ambao wako tayari kujitoa kwa vyovyote vile kujenga chama kama hiki na kutekeleza maazimio yake kwa heri ama kwa shari.

8. Mapinduzi ya Kidemokrasi ya Kitaifa (MKK)

Chama cha mapinduzi tunachokijadili hapa, pamoja na mambo mengine, kitakuwa na mbinu na hila za kupigania na kutekeleza mapinduzi ya kitaifa ya kidemokrasi. Shabaha ya mapinduzi ya kitaifa ya kidemokrasi, pamoja na mambo mengine, ni kuhakikisha kuwa nguvu za dola zinakuwa mikononi mwa wanamapinduzi, wafanyikazi na umma wa Kenya unaonyonywa na kugandamizwa

MKK yatatilia manani ukweli kwamba kadiri ambapo nchi yetu iko katika makucha ya ubeberu, kadiri ambapo uchumi wa kimsingi wa nchi yetu unatawalwa na wageni, mabepari wa nje, sisi wote Wakenya kwa ujumla, maskini na matajiri hatuko huru.

Aidha, MKK yatategemea wananchi wa Kenya wenyewe pamoja na bidii yao, uzalendo wao, ushujaa wao, usanii wao na uongozi bora wa kimapinduzi. Demokrasi ya umma inasema:

pasina nguvu za dola kuwa mikononi mwa umma unaopambania ukombozi kutoka kwa utawala wa kidikteta na ukoloni-mamboleo, hapawezi kukamilika MKK.

Tena, demokrasi ya umma, utawala wa wananchi wengi wanaopigania mageuzi ya kimaendeleo na ambao sasa wananyonywa na kunyanyaswa, unaoongozwa na wananchi wengi kwa ajili ya wananchi wengi na taifa letu, ndiyo shina na mizizi ya mapinduzi ya MKK.

Mabeberu wa kimataifa na vibaraka wao nchini hujitahidi kujaribu kutenganisha harakati za kidemokrasi na harakati za kitabaka. Ingawa katika hali halisi ya udikteta na ukoloni-mamboleo, kama katika nchi yetu sasa, wananchi wa tabaka mbalimbali wanaweza kuwa na umoja wa kupigania demokrasi na ukombozi wa kitaifa, hii si kusema kwamba harakati za kitabaka zinazimika. Harakati za kitabaka haziwezi kufichika wala kuzimika kadiri ambapo kuna matabaka nchini. Hakika hii ni kanuni halisi ya historia ya jamii ya binadamu.

Ndiyo kwa sababu, tabaka linalotawala, tabaka la wanyonyaji na vibaraka wa mabeberu, haliwezi kuongoza MKK. Bali chama cha kimapinduzi tunachokipendekeza, lazima kiunde mbinu halisi za kushirikisha wananchi wa makundi mbalimbali katika kupigania uhuru na demokrasi na kujenga uhuru na ukombozi wa kitaifa ikiwa ni pamoja na uchumi unaokua na kujiendeleza wa sekta za dola, ushirika na binafsi katika kipindi cha mpito.

Hili linaweza kufanywa kwa kuunda umoja wa kitaifa wa kupigania uhuru na demokrasi. Kwani kupambania uhuru na demokrasi ni kupambana dhidi ya ubeberu pia! Katika hali halisi ya Kenya, ambapo tuko chini ya utawala wa kishenzi na wa kiimla, ambao sasa umekua kama ufashisti, kupigania demokrasi ya kibepari ni kitendo cha kimaendeleo, kwani ni hatua mbele ya kuelekea kwa demokrasi ya umma.

9. Madai ya kidemokrasi ya umma wa Kenya sasa

Chama cha kimapinduzi tunachokipendekeza, sharti kiunge mkono kwa hali na kwa mali madai ya wananchi wengi wa Kenya wa kutoka matabaka mbalimbali ambayo ni pamoja na:

Kwanza, kuangushwa kwa imla wa Moi - Kanu kwa vyovyote vile. Kwani Wakenya wamejifunza kwamba hata bunge la sasa la 'vyama vingi' limeshindwa kabisa kuuondoa utawala wa kiimla ambao sasa umekua na unakaribia ufashisti.

Pili, kukomeshwa mara moja kwa vita vya dola dhidi ya wananchi. Serikali ya Moi inawaua maelfu kwa maelfu ya wananchi, kuvuruga uchumi wao na kuwafanya wakimbizi ndani ya nchi yao yenyewe kwa kisingizio cha vita vya kikabila na mfumo wa vyama vingi.

Tatu, kukomeshwa kwa siasa za kishenzi na za kupinga maendeleo za majimbo ya kikabila ambazo zina lengo la kuudumisha uimla, kuvunja taifa letu na kupanda mbegu za chuki za kikabila miongoni mwa wananchi wa Kenya. Moi na Kanu wanafanya njama za kuigeuza Kenya kuwa kama Yugoslavia ya zamani, Rwanda na Burundi ama Somalia.

10. **Kongamano Kuu ya Kitaifa**

Nne, kufanyika kwa Kongamano Kuu ya Kitaifa litakayojadiliana kuhusu Kenya mpya ya kidemokrasi inayopiganiwa na wengi wetu. Ni muhimu kutaja kwamba Kongamano Kuu la Kitaifa ni mbinu ya mapambano ya kidemokrasi ambayo inashirikisha makundi yote katika jamii yanayopambania demokrasi, umoja wa kitaifa na kupinga udikteta. Kwa sababu hii, Kongamano la Kitaifa linadai uongozi thabiti wa ujasiri, uliyo tayari kuitisha kongamano

yenyewe pasina idhini ya Moi na serikali yake, linahitaji uongozi uliyo tayari kuyatekeleza maazimio ya kongamano hilo kwa vyovyote vile, kwa heri ama kwa shari.

Kufanyika kwa Kongamano ya Kitaifa kutatokana na mapambano makali dhidi vyombo vya dola. Kwani kufanyika kwake kutatangaza sura mpya ya mapambano ya kidemokrasi Kenya kutumia mbinu za kidemokrasi. Maadamu kuitishwa kwa Kongamano la Kitaifa vilevile kuna maana kuwa wananchi hawana imani tena na serikali iliyoko na wanadai serikali badala.

Tano, Kongamano la Kitaifa litakuwa na jukumu, pamoja na majukumu mengine, ya kujadili na kuandika katiba mpya ya kitaifa ambayo itawasilishwa kwa raia kujadiliwa na hatimaye kupitishwa kwa kura za maoni. Kwani kama tulivyosema awali, katiba ya sasa ya kitaifa ni ya kikoloni, kidikteta na haiwezi kuwa mwongozo wa demokrasi na haki za binadamu.

Sita, kukuwepo kwa mfumo wa vyama vingi bila masharti yoyote kutoka kwa serikali. Tuna maana kwamba vyama vyote vya kisiasa vinavyotaka kujiandikisha viwe na haki ya kufanya hivyo kufungamana na katiba. Katiba mpya ya kitaifa, itakayopendekezwa na Kongamano la Kitaifa na kukubaliwa na wananchi wote wa Kenya kwa kura za maoni, ndiyo itakayoweka taratibu za kufuatwa na vyama vyote vinavyotaka kujiandikisha ambazo zitazingatia misingi ya kuimarisha demokrasi na uhuru wa kitaifa na haki za binadamu.

Saba, makundi mbalimbali ya kijamii Kenya kama vyama vya wafanyikazi, walimu, wanafunzi, wakulima, wasanii, wanawake, vijana, wafanyibiashara, wakodeshaji nyumba, wanunuzi, wachuuzi, wanamichezo, walemavu, na kadhalika navyo yaandikishwe na yawe na uhuru wa kufanya shughuli zao bila vikwazo.
Nane, wananchi watekeleze haki zao za kukutana, kusema na kusambaza maoni yao, kusafiri, kusoma kile wanachokitaka, kuabudu, kuandamana, kugoma kushiriki kikamilifu katika kujadili na kupitisha sera kuu za serikali zinazohusu maisha yao.

Tisa, wale wenye hatia za kuvunja haki za binadamu na kuiba mali ya umma washtakiwe na kuhukumiwa kufungamana na sheria.

Kumi, wafungwa wote wa kisiasa wafunguliwe mara moja na hatua madhubuti za kukomesha unyama wa polisi dhidi ya wananchi na ufashisti katika magereza na vituo vya polisi ukomeshwe mara moja.

Kumi na moja, mipango ya kiuchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, ambayo ni mipango ya kinyama na kibeberu inayokusudiwa kutunasa katika mitego ya kunyonywa na kufukarishwa kama taifa milele, nayo iwachwe kutekelezwa mara moja. Mipango hii ya IMF na Benki ya Dunia inasababisha kuondolewa kwa huduma muhimu za kijamii kama matibabu, elimu, nyumba na kadhalika. Mipango hii inayokusudiwa kujenga uchumi wa kibepari-kikoloni siku zote inasababisha kuzoroteka kwa uchumi, ukosefu wa ajira, umaskini, njaa, maradhi na kuongozeka kwa ufukara.

11. **Demokrasi ya kisoshalisti**

Mwisho, lengo la hatimaye la MKK ni kuelekeza Kenya katika barabara ya kujenga demokrasi ya juu zaidi kuliko ile ya kibepari, demokrasi ya kisoshalisti. Katika demokrasi ya kisoshalisti dola litakuwa mikononi mwa tabaka la wengi, wafanyikazi, wakulima makabwela na wazalendo, wanamapinduzi na wale wote katika jamii wanaonyonywa na kunyanyaswa na wanaopigania jamii ya haki na usawa kwa kila mwananchi. Kwa hivyo, demokrasi ya kisosashalisti ni demokrasi ya umma.

Demokrasi ya kisoshalisti ni ya kuwahamasisha wananchi wengi na kuwapa uwezo wa kiitikadi, kiuchumi na kisiasa wa kupambana dhidi ya ubepari na ukoloni-mamboleo, kuvunja mali ya binafsi na kuhakikisha kuwa njia kuu za uzalishaji, ardhi, viwanda na biashara kuu za ndani na nje ya nchi zinamilikiwa na dola, wazalishaji wenyewe na jamii kwa ujumla. Demokrasi ya kisoshalisti ina shabaha ya kuikata mirija ya unyonyaji wa mtu kwa mtu.

Demokrasi ya kisoshalisti ni utawala wa wengi wanaopigania maendeleo na mapinduzi ya kupambana dhidi ya wachache wanaopinga maendeleo na mapinduzi. Demokrasi ya kisoshalisti ni udikteta wa umma wa wafanyikazi, udikteta wa kuhakikisha ukombozi wa jamii kutoka kwa mfumo wa unyonyaji na ugandamizaji wa mtu kwa mtu.

Bali udikteta wa umma wa wafanyikazi ni tofauti na ule wa mabwana katika mfumo wa utumwa, makabaila katika mfumo wa ukabaila na mabepari katika mfumo wa ubepari. Kwani katika mifumo hii yote, watu wachache katika jamii, wanatumia nguvu za dola kuyadumisha mahusiano ya kikatili na kinyama ya unyonyaji na udhalimu wa mtu kwa mtu. Lakini katika usoshalisti, wengi katika jamii wanatumia nguvu za dola kuuondoa udhalimu na unyonyaji wa mtu kwa mtu, kufanya mahusiano ya kiuchumi ya kiutu na kimaendeleo, kujenga jamii mpya inayojali maslahi ya kila mtu. Kwa sababu hii, demokrasi ya kisoshalisti ni ya hali ya juu na ya kiadili zaidi kuliko zote.

Ndiyo kwa maana chama cha kimapinduzi tunachokipendekeza lazima kijitayarishe kinadharia na kimatendo kuwa katika msitari wa mbele wa kuwazatiti, kuwahamasisha na kuwaongoza wafanyikazi, wazalendo na umma kupigania na kutekeleza demokrasi ya umma. Wakati kikifanya hivyo, sharti wakati wote chama cha mapinduzi kizingatie msimamo wa kitabaka na itikadi ya kimapinduzi. Maana bila itikadi ya kimapinduzi hapawezi kuwa na harakati za kimapinduzi. Tena sharti kila mara tukumbuke kuwa demokrasi ya kibepari si alfa na omega ya demokrasi. Maana kuna demokrasi ya hali ya juu zaidi kuliko ya kibepari, demokrasi ya kisoshalisti ambayo ni demokrasi ya umma.

Vilevile, ni muhimu kama wazalendo, wanamapinduzi na taifa tuwe wabunifu katika kufafanua na kutekeleza demokrasi ya umma. Maana sharti demokrasi ya umma iwe na mizizi katika hali halisi ya nchi yetu, historia yetu na utamaduni wetu. Bora tuhakikishe kuwa demokrasi ya umma inashirikisha umma katika maswala yote yanayohusu maisha yao, yawe ya kiutawala, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, na kadhalika. Wala tusiwe makasuku wa kuiga demokrasi ya mataifa mengine. La muhimu ni kujifundisha kutoka mataifa mengine kuhusu kile ambacho tunastahili kujifunza na kile ambacho tunastahili kukiepuka ili tusije tukarudia historia. Na tunapojifunza kutoka kwa mataifa mengine tunazingatia hali halisi ya nchi yetu na historia yake. Wakati wote tuhakikishe kuwa demokrasi nchini inajenga na kutekeleza uhuru, haki za binadamu, usawa, amani; iwe ni demokrasi ya kuinua na kuwapa uwezo umma kwa kila hali kwa kujenga mazingira ya kushirikisha kila mtu katika jamii katika uzalishaji wa maendeleo na kunufaika kutokana na maendeleo yanayozalishwa. Shabaha ya demokrasi ya umma ni kumjenga binadamu mpya mwenye elimu na mwamko wa kutambua utu wake na kuathiri maumbile kwa uzuri. Yaani binadamu ambaye ni kiumbe huru, mwenye mwamko, mbunifu, mzalishaji na anayeishi katika jamii. Kwa muhtasari, demokrasi ya umma ni ya kupambania na kujenga usoshalisti na hatimaye ukomunisti.

Mwandawiro Mghanga, Uppsala, Sweden, Jumamosi 18 Oktoba 1997